Waebrania, Mlango Wa Saba [1]

. . .usiku, na kumsikia Joyce akiimba. Je! hivi mlijua ya kwamba huo wenyewe ni muujiza? Maskini msichana huyo mdogo, anawezaje kuwazia kuhusu hayo yote? Na kila usiku anatuimbia wimbo mpya. Anawezaje kuwazia kuhusu hayo yote, hiyo kweli ni akili ndogo hodari. Bwana na ambariki mtoto huyo.

2 Sasa, kesho, saa nane na nusu, kwenye nyumba ya wafiwa huko Charlestown, Indiana. Hayati dada yetu mpendwa, Dada Colvin, tunampa heshima za mwisho, kwenye ninii—kwenye nyumba ya wafiwa na pale kaburini, kesho alasiri. Mmoja ambaye wakati mmoja aliishi kama mnavyoishi ninyi usiku huu, naye amepita ng'ambo ya pazia ambako wewe utapita wakati mmoja. Na wote wanaotaka kuhudhuria ibada, mbona, mnakaribishwa kuja. Bila shaka itakuwa ni msaada mkubwa kwa familia ya Colvin, kujua ya kwamba maskani hii hapa, ambapo wote wamehudhuria kanisani kwa muda mrefu sana, na kadhalika, watahudhuria hayo mazishi. Tungefurahi kuwa na ninyi nyote kuhudhuria kule. Nami nadhani ninii . . .Ndugu yetu mpendwa McKinney, yule aliyehubiri kwenye mazishi ya ndugu yangu, miaka kadha iliyopita, ndiye anayeendesha sehemu muhimu kubwa ya mazishi hayo, nami nimeombwa kuhudhuria kumsaidia katika—katika ibada za mazishi.

3 Sasa, nilikuwa nimechelewa kidogo tu, usiku wa leo. Nina shughuli nyingi sana kwa wakati mmoja, sijui nifanye nini. Ninapigiwa simu nyingi sana, na wagonjwa wote hawa wa akili na ajali hizi za barabarani, huku watu wakipiga simu, wakija. Mpaka, ndiyo kwanza nitoke Louisville, muda mfupi tu uliopita, nipate kurudi hapa upesi, na nikaacha miito mingi ya simu ambazo zinachosha sana na ambazo bado hazina budi kupigwa, nadhani, usiku wa leo. Na sasa mtuombee tunapoendelea.

4 Na asubuhi ya leo kamwe si—sikufikia somo la—langu, kwenye mlango wa 7 wa Kitabu cha Wa—Waebrania. Na tukiwa tunakifungua, usiku wa leo, ninataka kutoa lile tangazo linalohusu mkutano wa Ndugu Graham Snelling, hapa juu kwenye lile hema hapa juu, mwishoni mwa Barabara Kuu ya Brigham. Bwana akipenda, ninataka kurudi Jumatano usiku. Na hapo tutaandaa usiku fulani ambapo tutaenda huko kama ujumbe, wakati fulani juma hili, kumtembelea Ndugu Graham kwenye mkutano huo. Naye ni ninii . . .anasema, "Ana kundi zuri." Na—na atafurahia kuhudhuria kwetu, kumsaidia. Ndugu

Graham Snelling, yeyote wenu anayehudhuria mkutano huo, ama anayetaka kuuhudhuria, ni hapo mwisho tu wa Barabara Kuu ya Brigham hapa juu. Mtu ye yote anaweza kukwambia mahali ulipo. Moja kwa moja mwishoni mwa viwanja vya michezo, ndipo hilo hema lilipo. Atafurahia ushirika wenu. Kwa sababu, sisi kama maskani tumeahidi ushirikiano wetu naye, asilimia mia moja, kwa hiyo tunajaribu kusaidia.

5 Sasa, ndipo hivi karibuni tunafikia kwenye sehemu ya, Bwana akipenda, kwenye mlango wa 11 wa Waebrania, katika siku chache usiku, Mungu akipenda, na hapo nafikiri tutakuwa na wakati mzuri sana pia.

6 Loo, Bwana alitubariki asubuhi ya leo katika njia ya ajabu sana, jinsi alivyommimina Roho Wake juu yetu! Na sasa, usiku wa leo, tunamtarajia kufanya jambo hilo tena; na halafu Jumatano usiku, na kuendelea. Na—na zile siku za usiku ninazokosekana, Ndugu Neville atakuwa hapa kuendelea moja kwa moja, endapo nimetoka.

7 Sijui kamwe nitakalofanya, mtu huenda ukawa hapa saa hii, na saa nyingine ukaitwa huko California. Unaona, hujui tu ni wapi Bwana atakakokutuma. Hiyo ndiyo sababu ni vigumu kwangu kufanya ratiba na kusema tuta—tutafanya *hivi na vile*. Ninaweza kuanza kufanya jambo fulani, Bwana atanituma mahali pengine. Unaona? Kwa hiyo hatujui kabisa atakalofanya. "Lakini Bwana akipenda," tulisema. Nafikiri tumeagizwa, ama tumeamriwa hivyo, katika Biblia, "Bwana akipenda, tutafanya mambo *haya na yale*." Kwa hiyo ikitokea kwamba hatufanyi miadi ya kwamba tutaninii . . . ama kutimiza miadi, tunajisikia ya kwamba labda Bwana hakutaka jambo hilo litukie.

8 Hivi majuzi, tulicheleweshwa, Ndugu Roberson na Ndugu Woods na mimi mwenyewe. Nasi tunashangaa, "Kwa nini?" Nilikuwa nimeketi pale, nikiangalia ramani, tukija moja kwa moja, nasi tukaendesha maili hamsini moja kwa moja kurudi kaskazini tena kwenye barabara moja. Nami nimekuwa nikisafiri kwenye barabara kuu tangu nilipokuwa na umri wa kama miaka kumi na minne. Nami ninashangaa jinsi nilivyopata kufanya hivyo. Tulikuwa tumesimama pale, sisi sote watatu. Sote tumesafiri kwenye barabara kuu. Nikiangalia moja kwa moja kwenye ramani, tukishikilia barabara ya 130, tukipitia Illinois, kisha tukapiga kona kidogo, bila ya kuwa na habari ya kwamba jua lilikuwa nyuma yetu badala ya kuwa usoni mwetu. Tulikuwa tukielekea kaskazini badala ya kusini. Na muda si muda unajua, tukavuka barabara, nikasema, "Hii siyo barabara yenyewe." Nikaangalia kule chini, ndipo nikakuta kwamba, tulikuwa tumetoka kwenye njia umbali wa maili hamsini. Tukawa tumerudi moja kwa moja nyuma . . .? . . .

9 Basi tuliporudi, tu—tulikuwa tukizungumza. Nikasema, "Mnajua ni kwa nini? Sisi . . . Huenda Bwana alitupitisha hivi,

kutuepusha na ajali mbaya sana huko chini mahali fulani, ambayo vinginevyo ingefanya jambo fulani. Tunajua ya kwamba mambo yote yanatendeka kwa ajili ya manufaa kwa wale wampendao Bwana. Hayo tu ndiyo tunayopaswa kukumbuka."

10 Sasa, usiku wa leo, tunaanza sasa kuendea somo fupi la mafundisho. Na kama ninaninii. . . Sidhani tutazama ndani, labda tutafikia usiku wa leo, kuninii. . . Huu ndio ule mlango muhimu sana wa mafundisho juu ya kutoa fungu la kumi, kwa kanisa. Na ni somo kubwa, ambalo tungeweza kudumu nalo kwa majuma kadha wa kadha, kwenye jambo hilo moja, jinsi ambavyo Ibrahimu alimtolea Melkizedeki fungu la kumi, na kama ni jambo la lazima.

11 Je! feni hii inamdhuru mtu ye yote huko nyuma? Mngetaka izimwe? Kama inamsubua mtu yeyote, ikimpulizia usoni mwao, feni yoyote hiyo. Kama inasumbua, inueni tu mikono yenu. Na, ama mtume tu mmoja wa mabawabu, mtume mtu fulani kwa ndugu huyu hapa, ataizima kwa ajili yako. Na kwa namna fulani mimi mwenyewe ninaizima; ninapata joto na kuanza kutoa jasho, halafu, muda si muda unajua, ni—ninapwelewa na sauti. Kwa hiyo, ni juu yenu, kwa hiyo haitanisumbua kwa njia yoyote. Tunataka mjisikie vizuri.

Hatutajaribu kuchukua muda wenu mwingi mno, bali tutaelekea moja kwa moja kwenye Neno. Na kabla hatujafanya hivyo, hebu na tuzungumze na mwandishi wake kwa muda kidogo tu.

12 Sasa, Baba wa Mbinguni, hatujui ni kitu gani kinachotungojea. Lakini jambo pekee tunalojua, na tumeshawishika, ni ya kwamba mambo mema yako mbele zetu. Kwa kuwa imeandikwa, "Jicho halijaona, wala sikio halijasikia, wala halijaingia mioyoni mwa wanadamu, yale Mungu aliyowawekea akiba, hao wampendao."

13 Nasi tunaomba ya kwamba utayafungua madirisha ya Mbinguni usiku wa leo, katika ghala Yako, na utupe Neno Lako, ambalo litakuwa ni jambo ambalo linafaa, jambo fulani la kuongeza imani yetu kama Wakristo, kutufanya tutulie za—zaidi katika Injili, kuliko tulivyokuwa wakati tulipoingia. Tujalie hilo, Baba. Jalia Roho Mtakatifu alichukue Neno la Mungu na kulileta kwenye kila moyo kadiri tunavyohitaji. Katika Jina la Mwanao mpendwa, Yesu, tunaomba. Amina.

14 Sasa, asubuhi ya leo, katika kuacha kifungu cha mwisho cha mlango wa 6, kusudi tuingie moja kwa moja kwenye wa 7.

> *Alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu, amekuwa kuhani mkuu hata milele kwa mfano wa Melkizedeki.*

15 Sasa tutasoma vifungu vitatu vya kwanza, ama vifungu viwili vya kwanza, ama vifungu vitatu vya kwanza, hasa, vya mlango wa 7, tupate kuanza mara moja.

Kwa maana Melkizedeki huyo, mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, akambariki;

Ambaye Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi ya vitu vyote, (huko hapo kutoa kwako fungu la kumi); *(tafsiri ya jina lake kwanza ni mfalme wa haki, tena, mfalme wa Salemu, maana yake, Mfalme wa amani;*

Hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku . . . hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu); huyo adumu kuhani milele.

16 Ni tamshi zuri jinsi gani! Sasa itatubidi kurejea kwenye Agano la Kale, tupate kuchimbua vinono hivi vikuu. Na, loo, jinsi ninavyovipenda!

17 Mnajua, huko Arizona, tulikuwa tukitafuta madini. Nasi tungefikia kwenye kipande cha ardhi kinachoonekana ni kizuri, mimi mwenyewe na Bw. Mc Anally. Nasi tungeona mahali ambapo ilionekana kana kwamba, katika mifereji midogo, ambamo pamenyonywa unyevu, kile wanachoita "ufulio." Nami ningeninii . . . Angefanya niiname na kunifanya nisugue changarawe halafu "whiu," ninaipulizia. Kisha ninazisugua halafu "whiu," ninaipulizia. Nami sikujua ni kwa nini alifanya hivyo. Nikaja kutambua, unaona, unapopulizia changarawe, ni nyepesi. Na yote, hata risasi, ni nyepesi kuliko dhahabu. Dhahabu ni nzito kuliko risasi. Kwa hiyo wakati unapopulizia, vyuma hivyo vingine vyote pamoja na changarawe na mavumbi vitapeperushwa, lakini dhahabu itabaki chini. Kwa hiyo, kama una ufulio kutoka *hapa* ndani, inaonyesha ya kwamba kuna mchirizi wa dhahabu mahali fulani huko. Mvua hii imeosha vipande hivi vidogo. Kwa hiyo basi, tunapopata vipande hivi na kadhalika, na tukichimba karibu kilima chote, tukijaribu kupata dhahabu hii. Tunachimba mashimo ardhini, tunayachimbua. Tunaweka baruti, tunalipua. Tunaendelea kulipua mashimo, tukiingia ndani mpaka tulipata, tunapata bamba lenyewe. Sasa, huko ndiko tunakoita "kutafuta madini."

18 Na usiku wa leo tunajaribu kulichukua Neno la Mungu, na kulitumia kwa nguvu za Roho Mtakatifu, kulipua kutokujali kote na mashaka vituondoke, vitu hivyo vyote vidogo vyepesi vilivyopambwa ambavyo havina msingi wo wote, visivyo na maana yoyote maishani mwetu, tunataka kuvilipulia mbali vyote ili kwamba tuweze kupata Bamba hili lenye utukufu. Bamba hilo ni Kristo.

19 Na sasa Mungu na atusaidie tunaposoma na kujifunza katika Neno Lake. Milango mitatu ya mwisho iliyotangulia, karibu hiyo yote, tumekuwa tukinena juu ya kusikia, mara kwa mara tu, Melkizedeki.

20 Sasa, nafikiri Paulo anatoa fasiri ya kweli.

Kwa maana Melkizedeki huyo, mfalme wa Salemu, . . .

"Mfalme wa Salemu." Na mwanachuoni yeyote wa Biblia anajua ya kwamba Salemu hapo awali ilikuwa . . . Yerusalemu hapo awali iliitwa "Salemu." Naye alikuwa ni Mfalme wa Yerusalemu. Mwangalie.

. . . kuhani wa Mungu aliye juu, (hiyo ni kusema mwombezi), *aliyekutana na Ibrahimu . . .*

Ninataka kuupata ukoo wake, Mtu huyu mashuhuri, mpate kujua Yeye ni nani, kwanza, na kisha mtaninii . . . tutaendelea na hiyo hadithi.

. . . alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, akambariki;

Ambaye Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi . . . kwanza . . . tafsiri ya jina lake kwanza ni Mfalme wa haki, . . .

Sasa angalia, "Haki." Sasa, tuna haki ya kujifanyia sisi wenyewe, tuna haki ya kujifanya, tuna haki iliyopotoshwa, za kila aina. Bali kuna haki moja halisi, na haki hiyo hutoka kwa Mungu. Na Mtu huyu alikuwa ni Mfalme wa haki. Yeye angeweza kuwa ni nani?

21 Sasa, Yeye alikuwa ni Mfalme wa haki, Mfalme wa Yerusalemu, Mfalme wa haki, Mfalme wa amani. Yesu aliitwa, "Mfalme wa amani." Na mfalme ni mwana wa mfalme. Kwa hiyo, Mtu huyu alikuwa ni Mfalme wa amani, ndipo hapana budi Yeye ni Baba wa Mfalme wa amani. Mnafahamu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

22 Sasa hebu na tuone, tupate ukoo Wake mbele kidogo, tuone mahali tunakoelekea.

Hana baba, . . .

Sasa, Yesu alikuwa na Baba. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika.

. . . alikuwa *hana mama, . . .*

Yesu alikuwa na mama. Bali Mtu huyu hakuwa na baba wala mama.

. . . hana wazazi, . . .

Hakuwa na mtu yeyote aliyetokea Kwake, wazazi wowote. Yeye daima alikuwako. "Hana wazazi."

. . . hana mwanzo wa siku zake . . .

Kamwe hakuwa na wakati alipoanza.

. . . wala mwisho wa uhai wake, . . .

Isingekuwa kitu kingine ila Mungu. Hivyo tu ndivyo ingaliweza kuwa.

23 Sasa, sasa kama mtaangalia tunaposoma kifungu kifuatacho. Unaona? "Kwanza, tafsiri yake, Mfalme wa haki." Hapo sipo ninapotaka kuendelea napo. Ki—kifungu cha tatu, "Wala mwisho wa uhai wake."

. . . bali amefananishwa na Mwana wa Mungu; . . .

Sasa, Yeye hakuwa Mwana wa Mungu, kwa kuwa, kama alikuwa ni Mwana, basi Yeye alikuwa na mwanzo. Wala Mtu huyu hakuwa na mwanzo. Kama alikuwa ni Mwana, ilibidi awe na baba na mama pia. "Wala Mtu huyu hakuwa na baba wala mama. Bali alifananishwa na Mwana wa Mungu."

. . . adumu kuhani milele.

24 Sasa, Dk. Scofield anajaribu kusema, ya kwamba, "Ilikuwa ni ukuhani, ulioitwa 'Ukuhani wa Melkizedeki.'"

Lakini ninataka kushindana nanyi juu ya jambo hilo kwa dakika chache tu. Kama ulikuwa ni ukuhani, basi ilibidi uwe na mwanzo, pia ilibidi uwe na mwisho. Lakini, "Huu haukuwa na mwanzo wala haukuwa na mwisho wo wote." Naye hakusema ya kwamba alikutana na ukuhani. Alikutana na Mwanamume, naye akaita jina lake "Melkizedeki." Yeye alikuwa ni Mtu, si madhehebu, si u—u—ukuhani au ubaba. Yeye alikuwa ni Mtu kabisa aitwaye Melkizedeki, aliyekuwa Mfalme wa Yerusalemu. Si ukuhani, bali ni Mfalme asiyekuwa na baba. Ukuhani hauna baba. "Na Mtu huyu hakuwa na baba, hakuwa na mama, hakuwa na mwanzo wa siku Zake wala mwisho wa uhai Wake." Sasa, Mwana wa Mungu . . .

25 Huyu alikuwa, alikuwa ni Yehova. Huyu alikuwa ni Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Asingekuwa mwingine.

26 Sasa angalia, "Anaishi milele." Ana ushuhuda hapa, ya kwamba, "Yu hai milele. Yeye hafi." Hajawahi kufa. Hajapata kamwe kuwa vinginevyo bali kuwa hai. "Anadumu milele."

27 Sasa, Yesu alifanywa, akafananishwa Naye. Sasa, sababu ya kuwako na tofauti kati ya Mungu na Yesu: Yesu alikuwa na mwanzo; Mungu hakuwa na mwanzo. Melkizedeki hakuwa na mwanzo, naye Yesu alikuwa na mwanzo. Lakini Yesu alifanywa, alifananishwa Naye. "Kuhani, adumu milele."

28 Sasa, wakati Melkizedeki alipokuwa hapa duniani, hakuwa kitu ulimwenguni ila yule Ye—yule Yehova Mungu aliyedhihirishwa kwa uumbaji, Yeye alikuwa hapa kama theofani. Ibrahimu alikutana Naye wakati mmoja, hemani mwake. Na kama tulivyosema asubuhi ya leo, "Ibrahimu alimtambua. Naye alimwambia Ibrahimu aliyokuwa anaenda kufanya, kwa kuwa hangemwacha mrithi wa ulimwengu asijue mambo ambayo alikuwa anaenda kuyafanya."

29 Hebu nisimame hapa kwa dakika moja, kusema, Mungu angali ana maoni yale yale kuhusu Kanisa Lake. Ninyi si watoto wa giza. Ninyi ni watoto wa Nuru. Na ninii . . . sisi ambao . . .

"Heri walio wapole, kwa kuwa watairithi nchi." Na je! Mungu, Ambaye alitenda kwa—kwa Ibrahimu, ambaye alikuwa airithi nchi. . . Naye alisema, "Sitamficha mambo haya mtu ambaye anaenda kuirithi nchi." Ni zaidi sana vipi atalifunulia Kanisa Lake siri Zake wale ambao watairithi nchi!

30 Danieli alisema, "Katika siku hiyo wataenda mbio huko na huko, maarifa yataongezeka." Kisha akasema, "Wenye hekima watamjua Mungu wao, katika siku hiyo, nao watafanya mambo makuu katika siku hiyo. Bali walio waovu hawatamjua Mungu wa Mbinguni." Wanamjua kwa desturi na kawaida za dini, kama vile somo letu la kwanza lilivyosema, bali hawamjui kwa njia ya ukamilifu.

31 Naye Mungu anaweza tu kufanya kazi kwa ukamilifu, kwa maana yeye ni Mkamilifu. Jina Lake lihimidiwe. Hapana budi iwe ni njia kamilifu ambayo Mungu anatendea kazi, maana Yeye hawezi kufanya kitu kingine ila kutenda kazi kwa ukamilifu. Hawezi kujichafua kwa njia yoyote. Na ndipo basi hiyo ndiyo sababu Yesu alikuja kuziondoa dhambi zetu, tupate kukamilishwa, kusudi Mungu apate kutenda kazi kupitia Kanisa Lake. Hapo ndipo siri inapolala.

Hapo ndipo ambapo ulimwengu ni mpofu. Hapo ndipo wanapotaka kusema, ya kwamba, "Umerukwa na akili." Hapo ndipo wanapotaka kusema, "Hujui unayosema."

Kwa sababu, "Mambo ya Bwana ni upuuzi kwa hekima ya ulimwengu huu. Lakini mambo ya ulimwengu ni ya kimwili kwa mwamini." Kwa hiyo, wewe ni mtu wa tofauti, unaishi katika mazingira tofauti. Wewe si wa ulimwengu huu tena. Umepita kutoka kwenye maisha haya ukaingia katika Maisha mapya.

32 Kwa hiyo, Mungu anafunua, si kwa ulimwengu, si kwa mwanasaikolojia, si kwa wahudumu wenye elimu, bali kwa mnyenyekevu wa moyo. Watu Wake walio wapole, Yeye atafunua siri za mambo makuu ya Mungu, kwao. Unaona jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

33 Sasa, sasa, Ibrahimu alikuwa aurithi ulimwengu. Kupitia Mzao wa Ibrahimu mataifa yote yabarikiwe. Kwa hiyo Mungu alishuka na kuzungumza naye, katika umbo la Mwanadamu.

Sasa, Mungu daima amekuwapo duniani. Mungu kamwe hajaondoka duniani. Kama kamwe akiondoka duniani, sijui dunia ingekuwaje. Bali Mungu daima amekuwapo hapa katika umbo fulani. Loo, Jina Lake lisifiwe!

34 Yeye alikuwa pamoja na wale wana jangwani, wakitoka Misri, akiwa katika mfano wa Nuru. Alisema na Ibrahimu katika umbo la Mwanadamu. Alisema na Musa katika mfano wa Mwanadamu. Alisema na Kanisa katika umbo la Mwanadamu, Mwanawe, Kristo Yesu.

Naye anazungumza kupitia Kanisa Lake siku hizi, kupitia Kanisa lililotiwa mafuta la Mungu aliye hai, kupitia vyombo vya udongo. "Ninyi ni matawi. Mimi ni Mzabibu." Mungu angali anazungumza, na ulimwengu unamwona Yesu jinsi wewe unavyomwakilisha. Hivyo ndivyo ulimwengu ulivyoninii . . . "Ninyi ni nyaraka zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote." Maisha yako yanaonyesha kile ulicho wewe.

35 Sasa, huyu Ibrahimu akienda zake, akirudi. Tutarudi nyuma na kusoma habari zake, kwa dakika chache tu, katika Kitabu cha Mwanzo. Katika mlango wa 14 wa Mwanzo, ninaamini ndipo. Loo, jinsi hadithi hii inavyopendeza hapa! Sasa, sote tunajua habari za Ibrahimu, jinsi ambavyo Mungu alimwita kutoka katika nchi ya Wakaldayo na katika mji wa Uri, na kumwambia ajitenge na marafiki zake.

Mungu anapowaita wanaume ama wanawake, anataka utengano.

36 Sasa, hiyo ndiyo shida ya makanisa siku hizi, hawataki kujitenga na imani za kale za kimwili . . . wasioamini. Hiyo ndiyo sababu hatuwezi kusonga popote mbele. Tunaingia tu kwenye huo mtiririko mmoja wa kimwili, nasi tu—tunasema, "Loo, Jim ni jamaa mzuri, kama akinywa. Kama akininii . . . Nami ninaenda pamoja naye kwenye chumba cha kuchezea kamari, ila mimi sichezi kamari. Ni—ni—ninaenda pamoja na huyo msichana kwenye karamu. Wanazungumza mizaha michafu, na kadhalika, bali mimi sifanyi yoyote."

37 "Tokeni kwao." Hiyo ni kweli. "Jitengeni nao. Msiguse vitu vyao vilivyo vichafu, Nami nitawapokea," asema Bwana. "Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, msifungiwe nira pamoja na wasioamini." Msifanye jambo hilo. Jitengeni.

38 Naye Mungu alimwita Ibrahimu ajitenge na jamaa yake yote, na kutembea pamoja Naye. Ndugu, wakati mwingine inamaanisha kuondoka kwenye kanisa. Ilimaanisha hivyo kwa Paulo. Ilimbidi kuliacha kanisa lake. Ilimaanisha hivyo kwa wengi. Mara nyingine inamaanisha kuondoka nyumbani. Mara nyingine inamaanisha kumwacha baba na mama, na kuacha vyote. Simaanishi kusema huwa hivyo kila wakati, lakini mara nyingi ndivyo ilivyo. Ina maana kwamba inakubidi kuondoa kila kitu kati yako na Mungu, na utembee pamoja Naye peke yako. Loo, huo ushirika mtamu, uliobarikiwa, huo ushirika unaokuwa nao unapotenga kitu chako, nafsi yako, na vitu vya ulimwengu na waamini wa kimwili wanaokufanyia mzaha, na utembee peke yako pamoja na Kristo!

39 Ni mara ngapi ambapo nimemshukuru Mungu! Yeye alisema, "Nitakupa baba na mama katika ulimwengu huu wa sasa. Nitakupa marafiki na wandani. Nami sitakuacha kamwe, wala sitakupungukia. Hata ingawa ulimwengu wote ukikupa kisogo, nitaenda pamoja nawe, hata mwisho wa safari."

40 Ni majaliwa ya baraka jinsi gani, ya kwamba mwanadamu ana hiyo changamoto ya kumfuata Bwana Yesu, kujitenga na wandani wake wote wa kimwili, kumfuata Bwana. Na kama mtu yeyote anaonekana hajiheshimu impasavyo, na kuishi kama Wakristo, bali wanapenda mambo ya kimwili, ni bora kwako kumtafuta rafiki mwingine mara moja. Naam. Na kama hakuna mtu atakayetembea pamoja nawe, kuna Mmoja aliyeahidi kutembea pamoja nawe. Huyo ni, Bwana Yesu mwenye kuhimidiwa, Yeye atatembea pamoja nawe.

41 Mungu alimwambia Ibrahimu kuninii, "Jitenge." Na Ibrahimu akiwa mwanadamu tu kama alivyokuwa, alimchukua babaye akaenda naye, akamchukua mwana wa nduguye akaenda naye, mpwake; wote wakimning'inia. Na Mungu kamwe hakumbariki mpaka alipofanya vile Mungu alivyomwambia afanye.

42 Sisemi ya kwamba wewe si Mkristo. Kwa kusema hivyo, mimi simwondolei mtu yeyote Ukristo wake. Bali nitasema hivi, ya kwamba kama Mungu alikwambia jambo fulani la kufanya, Yeye hatakubariki kamwe mpaka utakapolifanya. Niko mimbarani usiku wa leo nikishikiliwa na moja ya mambo hayo juu yangu. Mikutano yangu haijakuwa jinsi inavyopaswa kuwa, kwa muda wa miaka miwili iliyopita. Ni kwa sababu nimemkosea Bwana. Yeye aliniambia, "Nenda Afrika, kisha uende India." Hili hapa, limeandikwa papa hapa, nyuma ya Kitabu hiki, sasa hivi.

43 Meneja aliniita, akasema, "Achana na hao Makaburu. India iko tayari."

44 Roho Mtakatifu alikutana nami, akasema, "Utaenda Afrika kama nilivyokwambia."

45 Ndipo mwaka mwingine ukapita. Nao mameneja... nilisahau jambo Hilo. Akasema, "Tunaenda India. Tikiti tayari ziko hapa."

46 Nikaanza kwenda, nikasahau jambo hilo mpaka nilipofika Lisbon. Usiku mmoja, ambapo, nilidhani nilikuwa ninakufa. Kesho yake asubuhi nikaanza, nikaingia bafuni, nikaoge. Loo, nilikuwa ninaumwa sana, ilikuwa vigumu kwangu kusimama. Hapo, hiyo Nuru ikining'inia pale bafuni, kasema, "Nilifikiri nilikwambia, 'Nenda Afrika, kwanza.'"

47 Mikutano yangu imekuwa ikififia tangu wakati huo. Ingawa nilienda India, kukiwako na karibu nusu milioni waliokuwa wamesimama pale, bali hilo halikuwa ni kufanya yale Mungu aliyosema nifanye. Ninajisikia ya kwamba mikutano yangu kamwe haitafanikiwa mpaka nitakaporudi moja kwa moja na kulisahihisha jambo hilo. Haidhuru nifanye nini, ni Afrika, kwanza, maana inakubidi kufanya hivyo. Hilo hapo Neno la Milele la Mungu, limelala pale. Nilijua jambo hilo vizuri sana. Bali sina budi kurudi. Nami ninajisikia ya kwamba mwaka huu

ujao ndio wakati ambao nitajikokota nitoke kwenye ganda, kwa msaada wa Bwana.

48 Injili hii tukufu ya kale ambayo imekuwa ikikua kwa urahisi, kama mwaloni, bali ninaamini iko tayari kutandaza matawi yake sasa. Ninaamini jambo Hilo, Ujumbe huu mkuu na jambo kuu. Ninaamini ya kwamba Bwana atatujalia kuutikisa ulimwengu mara nyingine tena kwa utukufu wa Mungu.

49 Inakulazimu kufanya yale Mungu aliyokwambia ufanye. Basi Ibrahimu akaendelea moja kwa moja, akachukua jamaa zake pamoja naye. Aliwapenda. Huo ni wajibu wa binadamu. Lakini baada ya kitambo kidogo, mwishowe, baba yake akafa naye akamzika. Halafu alikuwa na mpwake, ndipo ugomvi na ubishi ukatokea. Na, hatimaye, Lutu akachukua chaguo lake na akashuka akaenda Sodoma. Na unamwona Ibrahimu, hakuzozana na Lutu. Alisema, "Sisi ni ndugu. Haitupasi kubishana. Bali inua kichwa chako nawe uelekee upande wowote unaotaka kwenda. Ukienda mashariki, mimi nitaenda magharibi. Ukienda kaskazini, nitaenda kusini." Huo ndio msimamo wa Mkristo, kuwa tayari kumpa huyo mtu mwingine kilicho bora zaidi. Daima kiweke mbele zake, acha ajichagulie.

50 Kwa nini? Ni kitu gani kilichomfanya Ibrahimu kufanya jambo hilo? Alijua ya kwamba aliahidiwa na Mungu ya kwamba atarithi kitu chote kizima, hata hivyo. Amina. Kwa hiyo, basi, hema au kibanda, tunajali nini? Kitu hicho chote ni chetu. "Heri walio wapole kwa kuwa watairithi nchi." Yote ni yetu. Mungu alisema hivyo. Kwa hiyo mpe mtu huyo chaguo lililo bora zaidi, kama anataka. Labda hicho ndicho tu atakachowahi kupata. Lakini yote ni yenu, ninyi warithi wa wokovu kwa ahadi. Yote ni yenu.

51 Kwa hiyo, Sara, mwanamke aliyekuwa mzuri kuliko wote nchini, aliketi pale kwenye mimba ya kilima pamoja na mumewe kama alivyopaswa kufanya. Alivaa mavazi ya kawaida, naam, huenda alikuwa amevaa nguo za kawaida za kaliko, ama vyovyote mnavyotaka kuiita. Ambapo, Bibi Lutu alivaa kama milionea. Naye mumewe alikuwa ndiye meya wa hilo jiji. Naye alikuwa ni hakimu aliyeketi kwenye lango. Huyo mama alikuwa na kila kitu; alihudhuria mashirika yote ya kushona na karamu za kadi zilizokuwa zikiendelea huko Sodoma na Gomora. Bali Sara alifurahia zaidi kuishi pamoja na mumewe kwa riziki ndogo, na kujua ya kwamba alikuwa katika mapenzi ya Mungu, kuliko kufurahia utajiri wa . . . ama anasa za utajiri kwa kipindi kidogo. Hiyo ni kweli. Huo ndio wakati Mungu anapowazuru.

52 Na siku moja, wewe, kwa hakika tu kama unavyoendea njia mbaya, itakuingiza shidani siku moja. Unaweza kufikiri utakuwa sawa. Unaweza kufikiri unaepuka, bali huepuki. Inaweza kuonekana kana kwamba yote yamefunikwa, bali hayajafunikwa. Mungu anajua kila kitu. Anajua kama kweli

unamaanisha kwamba ungamo lako ama humaanishi. Anajua kama kweli unamaanisha kwamba unamwamini Yeye na umeokoka, na umemkubali Yeye, na umekufa kwa mambo ya ulimwengu, na u hai katika Kristo. Yeye anajua hayo.

53 Sasa, tunaona Ibrahimu, ninawataka mwone roho hii halisi. Loo, jambo lote lililobarikiwa hapa ni neema. Ninawatakeni msome pamoja nami sasa kutoka katika mlango wa 14 wa . . . Kutoka, hebu kidogo mara moja.

54 Sasa, jambo la kwanza lililotukia wakati walipofika kule chini, Lutu aliingia katika shida. Kwa nini? Yeye alitoka katika mapenzi ya Mungu. Na unapoingia katika shida wakati uko katika mapenzi ya Mungu, Mungu atakusaidia kutoka. Bali kama uko katika shida, nje ya mapenzi ya Mungu, kuna jambo moja tu la kufanya, rudi katika mapenzi ya Mungu tena.

55 Sasa, wafalme wote walikusanyika pamoja, nao wakatambua kwamba nyanda hizo kule chini zilikuwa na maji mengi, nao wangeshuka tu na waende wakaiteke maskini Sodoma hii chafu, Gomora, waiteke. Nao wakafanya hivyo. Ndipo waliposhuka na kuiteka, walimchukua Lutu pamoja nao.

56 Basi nataka mmwone Roho wa Kristo hapa katika Ibrahimu. Sasa angalia kifungu cha 14.

> *Ibrahimu aliposikia ya kwamba nduguye . . .* (Mnalipata?) . . . *nduguye ametekwa mateka, akawapa silaha vijana wake, waliozaliwa katika nyumba yake, watu mia tatu na kumi na wanane; akawafuata mpaka Dani.*

57 Loo, ni wazo lililobarikiwa jinsi gani la neema! Ibrahimu, wakati ndugu yake, ingawa alikuwa ameanguka kutoka katika neema, ingawa alikuwa katika hali hii ya kurudi nyuma; wakati aliposikia ya kwamba ulimwengu ulikuwa umemshika, na ulikuwa umemshika na kumteka mateka, wapate kumwua, Ibrahimu alitenda kwa Roho ya Kristo. Alikuja na kuwapa silaha wanaume wake waliozaliwa nyumbani mwake, na wakawafuata, na kuwafuatilia mpaka Dani. Na Dani ndio sehemu ya mwisho ya Palestina, "Dani hata Beer-Sheba," kutoka upande mmoja hadi mwingine. Na ni mfano wa Kristo, wakati aliopoona ya kwamba ulimwengu ulikuwa umechukua . . . ulikuwa umeanguka, kwamba alimfuata adui hata mwisho, apate kuirudisha jamii ya Adamu iliyoanguka.

58 Ninawataka mwangalie kifungu kinachofuata, jinsi linavyofurahisha Roho anavyonena hapa kupitia kwake. Vema, kifungu cha 15 sasa.

> *Naye akarudisha mali zote* (zote); *akamrudisha na Lutu nduguye na mali zake, na wanawake pia, na watu.*

59 Wakati Ibrahimu alipomfuatilia adui aliyekuwa amemchukua ndugu yake mateka, alimfuata kote nchini, mpaka

Dani, naye akarudisha kila kitu alichokuwa amepoteza katika lile anguko.

60 Ni picha nzuri jinsi gani ya Kristo, aliyesikia kutoka Mbinguni ya kwamba tulikuwa tumepotea naye akaja na kumfuatilia adui, kote kote mpaka kuzimu, naye akawashika watu waliopotea na kuturudisha na kuturejeshea kila kitu tulichokuwa nacho kabla ya lile anguko! Sisi, waliorudi nyuma, sisi tuliozaliwa kuwa wana wa Mungu, ambao tumepotoshwa tukawa wana wa Ibilisi, na kufanywa, na tukayafuatilia mambo ya ulimwengu, na kufanya makosa, na kukimbia kwa pupa kama Lutu alivyofanya, tukiuza haki zetu za wazaliwa wa kwanza na kuyafuatilia mambo ya ulimwengu. Kristo alishuka. Ingawa tulikuwa tumeanguka; Mungu, akijua hapo mwanzo ni nani angeokolewa na ni nani asingeokolewa, hivyo basi alishuka na kumfuatilia adui maishani kote, katika mauti, katika paradiso, akaingia kuzimu. Na kote kote kutoka Utukufuni kuingia kuzimu, naye akazishinda ngu—nguvu za kuzimu, na kumnyang'anya Ibilisi funguo, kisha akafufuka tena, na kuwarudishia wanadamu, hivi kwamba wanadamu apate kuwa mwana na binti za Mungu tena.

61 Unaona Roho iliyokuwa ndani ya Ibrahimu pale, Roho wa Kristo akija pamoja naye?

62 Sasa nataka mwone mbali kidogo, tunaposoma.

> *Abramu aliporudi kutoka kumpiga mfalme huyu Kedorlaoma na. . .wafalme waliokuwa pamoja naye, mfalme wa Sodoma akatoka amlaki katika bonde la Shawe, nalo ni Bonde la Mfalme.*

63 Walitoka wakaenda. Mfalme wa Sodoma alirudishwa. Ndugu yake alirudishwa. Watoto walirudishwa. Na hawa hapa wafalme wakatoka kwenda kumlaki. Na, pia, hapa ndipo ninapotaka kupafikia, ujumbe sasa. Angalieni hapa.

> *Na—na Melkizedeki mfalme wa Salemu (*Mfalme wa Yerusalemu, Mfalme wa amani) *akaleta mkate na divai, naye alikuwa kuhani wa Mungu Aliye juu sana.*
>
> *Akambariki, akasema,* Ibrahimu *na abarikiwe na Mungu Aliye juu sana, Muumba wa mbingu na nchi.*

64 Melkizedeki, Mfalme wa Salemu, pia alijiwakilisha Mwenyewe miongoni mwa wale wafalme hao wengine. Pia angalia, vita vilikuwa vimekwisha, Roho wa Mungu katika Ibrahimu, wa Kristo, aliyekuwa amemrudisha ndugu yake aliyepotea, kisha akamrudisha mahali pake sahihi, kwa yote aliyokuwa amepoteza. Aliyarudisha yote. Ndipo alipofanya hivyo, alitoa mkate na divai, ushirika. Hivi huwezi kuona kwamba huyo Melkizedeki alikuwa ni nani? Ilikuwa ni Mungu. Alileta ushirika, baada ya vita.

65 Sasa hebu tufungue tena, katika Mathayo 26:26, upesi sana, na tuone vile Yesu alivyosema hapa juu ya jambo hilo. Katika Kitabu cha Mathayo, mlango wa 26 na pia kifungu cha 26, tunataka kusoma kidogo tu hapa. Vema, Mathayo 26:26.

> *Kisha Yesu akaenda pamoja nao mpaka bustani iitwayo* Golgotha, Golgotha...ama *Gethsemane,* namaanisha, *akawaambia wanafunzi wake, Ketini hapa, hata niende kule kuomba.*

66 Ninaamini nimefungua Andiko lingine. Mathayo, ishirini... kifungu cha 26 cha mlango wa 26. Kama mtu yeyote amepapata, nisomee, kama u—kama unaweza kupapata. Ngoja kidogo. Huu ni mfano mzuri hapa. Sitaki mpakose. Naam. Huyo amepapata, dada.

> *Nao walipokuwa wakila, Yesu alitwaa mkate, akabariki,...*

Ilikuwa ni kitu gani? Vita vilikuwa vimekwisha.

> *...akaumega, akawapa wanafunzi wake, akasema, Twaeni, na mle; huu ndio mwili wangu.*

67 Unamwona huyo Melkizedeki? Mamia ya miaka hapo nyuma, alipokutana na Ibrahimu, baada ya vita kwisha, Yeye alimpa mkate na divai. Na hapa Yesu anawapa wanafunzi, baada ya vita Vyake vikali kwisha, Yeye aliwapa mkate na divai. Angalia. Angalia kule Kuja kwa usoni.

> *Akakitwaa kikombe, aka—akashukuru, akawapa, akisema, Nyweni nyote katika hiki;*
>
> *Kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano jipya, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa...dhambi na ondoleo la dhambi;*
>
> *Lakini nawaambieni, Sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu.*

68 Tuko vitani sasa. Tunamfuatilia ndugu yetu aliyeanguka, ambaye Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alimwona na kumchagulia Uzima wa Milele. Na mambo ya ulimwengu yamemnasa katika upepo wa kisulisuli. Yeye yuko huko ameendea mashirika na makundi mbalimbali, yeye na mke wake, wakienda huku na huko mitaani, wakivuta sigara na kunywa pombe na kufanya sherehe za ulevi, wakijaribu kupata amani. Naye Roho wa Kristo akiwa ndani yetu, kama vile angalikuwa katika Ibrahimu, tunamfuatilia. Tukiwa na silaha zote za Mungu, Malaika wa Mungu wakiwa wametuzunguka, tunaenda kumrudisha ndugu yetu aliyeanguka.

69 Na hatimaye vita vitakapokwisha, tutakutana na Melkizedeki tena, Mungu ahimidiwe, aliyembariki Ibrahimu pale, na akampa baraka, na kumpa mkate na divai, ushirika. Na wakati vita vitakapokwisha, tutakutana Naye. Sisi ambao ni

warithi wa ahadi ya Ibrahimu, warithi pamoja na Kristo katika ule Ufalme, tutakutana Naye mwishoni mwa safari, na kushiriki mkate na divai, tena, vita vitakapokwisha.

70 Huyo Melkizedeki ni nani? "Yule asiyekuwa na baba, hakuwa na mama, hakuwa na mwanzo wa siku zake wala mwisho wa uhai wake." Atakuwapo pale kutupa ushirika tena. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

71 Tunaposimama huku, katika siku fulani usiku, tunapokusanyika pamoja na kula ushirika kutoka katika mikono ya wahudumu, ikiwakilisha ya kwamba tunaamini katika mauti, kuzikwa, na kufufuka kwa Bwana Yesu, pa—pazia lile, mwili Wake aliokuwa amefunikwa nao, Mungu. Tunakua, kama uwakilisho, "Tumekufa kwa mambo ya ulimwengu, na tumezaliwa upya kwa Roho." Nasi tunatembea pamoja na Mwili wa Kristo, waaminio wote pamoja.

72 Wakati vile vita vikali vitakapokwisha, na tunakuja tena pamoja na Kristo, tutakula ushirika pamoja Naye katika Ufalme wa Mungu, upya; na kula nyama, na kunywa damu ya mzabibu tena, katika Ufalme wa Mungu. Loo! Huyo hapo Melkizedeki. Ndivyo alivyokuwa.

73 Sasa hebu na tusome mbele kidogo tu kumhusu Yeye hapa, na kifungu cha 18.

> *Na Melkizedeki mfalme wa Salemu akaleta mkate na divai,*. . .(Mnalipata?). . .*naye alikuwa kuhani wa Mungu Aliye juu sana.*
>
> *Akambariki, akasema,* Ibrahimu *na abarikiwe na Mungu Aliye juu sana, Muumba mbingu na nchi.*
>
> *Akambariki,*. . .*akambariki*. . .
>
> *Ahimidiwe Mungu Aliye juu sana, aliyewatia adui zako mikononi mwako. Abramu akampa fungu la kumi la vitu vyote.*

Alimtolea Melkizedeki fungu la kumi. Ibrahimu alimpa fungu la kumi la nyara.

74 Sasa ninataka mwangalie hapa wakati Paulo akiendelea, tukiweka msingi kwa ajili ya somo lijalo sasa.

> *Mfalme wa Sodoma akamwambia* Ibrahimu, *Nipe mimi hao watu, na hizo mali uchukue wewe.*

Sasa, mfalme wa Sodoma alisema, "Sasa, hebu nirudishie tu raia wangu, na mali uchukue wewe."

> *Ibrahimu akamwambia mfalme wa Sodoma, Nimeinua mkono wangu kwa* B*WANA*, *Mungu Aliye juu sana,*. . .
>
> *El Elion,* "anayemiliki mbingu na nchi," pale.
>
> . . .*Mungu Aliye juu sana, Muumba mbingu na nchi,*
>
> *Ya kuwa sitatwaa uzi hata gidamu ya kiatu*. . .

Hakuwa na uamsho mkubwa wa kukusanya pesa. Alimtaka tu ndugu yake aliyeanguka.

> . . .*wala cho chote kilicho chako, usije ukasema, Nimemtajirisha* Ibrahimu*;*
>
> *Isipokuwa hivyo walivyokula vijana, na sehemu za watu waliokwenda nami,* . . .

75 Sasa, ninawataka mwone, Ibrahimu alisema, "Sitatwaa uzi wala gidamu ya kiatu." Yeye hakupigana vita, kupata fedha nyingi sana. Na vita halisi vya kweli havifanywi kwa nia za kichoyo. Vita havipiganwi kwa ajili ya fedha. Vita hupiganwa kwa—kwa ajili ya nia, kwa msimamo. Watu hupigana vita kwa ajili ya maadili. Na wakati Ibrahimu alipotoka akaenda kumchukua Lutu, hakutoka akaenda ati kwa sababu alijua angewapiga hao wafalme na kuchukua mali zao zote, alitoka akaenda kwa ajili ya kanuni ya "kumwokoa ndugu yake."

76 Na mhudumu yeyote aliyetumwa chini ya uvuvio wa Mfalme wa Mbinguni, hataenda kutafuta pesa; wala hataenda kuanzisha makanisa makubwa, wala hataenda kuwasha moto wa madhehebu. Yeye ataenda tu kwa ajili ya uadilifu mmoja, na huo ni, "Kumrudisha ndugu yake aliyeanguka." Kama atapata hela moja katika matoleo ama kama hapati, haitaleta tofauti yoyote kwake.

77 Kama ninavyosema, "Vita halisi hupiganwa na kuendelezwa kwa maadili wala si kwa ajili ya fedha." Na wanaume na wanawake wanaojiunga na kanisa na wanaokuja kanisani, wapate kupendwa sana na watu, kwa sababu akina *Jones* ni washiriki wa hapo, ama wanabadilisha kanisa lao kutoka kanisa lililo dogo kuwa kanisa lililo kubwa, unafanya jambo hilo kwa nia ya kichoyo wala maadili ya kweli hayapo nyuma yake. Unapaswa uwe radhi kusimama kwenye mstari wa mbele wa vita.

78 Katika maskani hii hapa, mambo yanapoenda mrama, na ninyi wanaume na wanawake mtakaokimbia mwende mahali pengine, ama mkae nje mpaka huo mzozo mdogo ama ubishi umekwisha, kuna jambo kasoro kwenye tukio lenu. Kweli.

79 Tuna desturi hapa. Tuna u—tuna utaratibu hapa. Kanisa hili limewekwa msingi juu ya kanuni za Biblia. Kama kuna mtu hapa asiyefanya yanayofaa, nawe unafikiri hawafanyi, mwendee ukazungumze naye. Kama huwezi kumpatanisha, basi chukua ndugu fulani waende nawe, mmoja ama wawili zaidi. Kama hatapatanishwa basi, basi liambie kanisa. Na kanisa litamfukuza, wasiwe na ushirika pamoja naye. Na Yesu alisema, "Lolote mtakaloachilia duniani, nitaliachilia Mbinguni."

80 Hiyo ndiyo sababu mna shida nyingi sana, kwa kuwa hamzifuati kanuni za Biblia. Kama mtu fulani kanisani anasababisha machafuko, au jambo fulani linaenda vibaya, si kazi yako kwenda kumsengenya mwanamume huyo ama

mwanamke huyo. Ni kazi yako kumwendea mwanamume huyo au mwanamke huyo, na umwambie kosa lake. Na endapo hatakusikia, chukua mtu mwingine mwende naye. Asiposikia hao, basi kanisa linamwachilia. Yesu alisema, Lolote mtakalolifungua duniani, nitalifungua Mbinguni. Lolote mtakalolifunga duniani, nitalifunga Mbinguni." Hayo ndiyo mamlaka ya kanisa.

81 Hapa si muda mrefu uliopita, mhubiri mzuri rafiki yangu, alikuwa na mvulana, na mvulana huyo alikuwa akienda kanisani, kanisa lake mwenyewe. Ilifikia mahali alipoanza kuzurura na maskini msichana mmoja aliyevuta sigara na kunywa na kufanya yasiyofaa. Mhubiri akasema, "Bila shaka, hiyo ni kazi yake." Rafiki msiri wangu sana, na mvulana mzuri. Lakini alipumbazwa sana na kijana mwanamke fulani; naye alikuwa ameisha olewa, alikuwa na watoto, mumewe alikuwa yu hai. Alihofu wataninii. . .mvulana huyo angemwoa. Kwa hiyo, ndugu huyo alikuwa amehuzunika sana. Naye akaniambia, "Ndugu Branham, ninataka uende kwa mvulani *huyu* wangu. Ninataka umzungumzie."

82 Nikasema, "Ndugu. . ." karibu nilitaje jina lake. "Una njia bora zaidi. Usinitume. Kama mvulana huyo haishi maisha mazuri, na kanisa limemwona akifanya mambo mabaya, basi ni jukumu la kanisa linapaswa kufanya kazi hii. Hiyo imeachiwa kanisa. Nalo kanisa linaenda kule na kumwambia."

83 Kwa hiyo akamchukua ndugu fulani, na akaenda kule na kumwambia. Ndipo akamuudhi ndugu huyo, akamfahamisha ya kwamba alikuwa ashike lake, naye basi na afanye vivyo hivyo. Akamchukua ndugu mwingine, wawili zaidi, mashemasi wawili wakaenda kule na kumwambia mvulana huyo. Asingesikiliza jambo hilo. Wakaliambia kanisa. Naye hakuja kamwe kwa siku kadha usiku, apate kupatanishwa na kanisa baada ya dhambi yake kutajwa mbele ya kanisa. Ndipo basi, kanisa likamwachilia.

84 Na yapata mwezi mmoja tangu wakati huo alishikwa na nimonia, naye daktari akasema, "Hakuna uwezekano duniani hapa kwake kuishi." Ndipo akatambaa akarudi. Mungu anajua jinsi ya kufanya jambo hilo.

85 Tunajaribu kufanya jambo hilo sisi wenyewe, "Loo, unapaswa kumfukuza *fulani nafulani* kanisani. Unapaswa kufanya *hivi, vile*, ama *vinginevyo*." Je! mmetekeleza sehemu yenu kama kanisa juu ya jambo hilo? Haya basi. Hiyo ndiyo njia ya kuwafanya watambae warudi, kuwaachilia kwa Ibilisi wakati mmoja.

86 Paulo alisema nini juu ya mtu huyu kule aliyekuwa akiishi na mama yake wa kambo? Wasingeweza kumpatanisha. Kasema, "Mtoeni kwa Ibilisi." Angalia kinachotukia. Na katika waraka huo mwingine alioandika Paulo, mtu huyu alikuwa amejiweka

sawa. Hakika. Mungu ana njia ya kufanya mambo haya, kama tu tutazifuata kanuni Zake.

87 Kama kitu fulani kikienda kombo kanisani, kama ni miongoni mwa kusanyiko, kila mmoja wenu ninyi ndugu. Kama ni kwenye halmashauri ya mashemasi, mmoja wenu ninyi mashemasi anaenda vibaya, hao washemasi wengine wanakuja na kufanya mkutano, kujaribu kumpatanisha ndugu huyo, kumwambia yale anayofanya; ama mmoja wenu ninyi washiriki, hata uwe ni nani. Ndipo linapaswa liletwe mbele zake. Kama hatafanya jambo hilo, basi njoni mmwambie mchungaji. Ndipo, anaachiliwa kutoka kwenye kanisa, na ndipo acheni awe kama kafiri na mtoza ushuru. Ndipo mwangalie Bwana akianza kumfanyia kazi. Unaona, hapo ndipo anapojirudia. Hapo ndipo anaporudi akitambaa. Bali tunajaribu kufanya jambo hilo sisi wenyewe, mwajua, tunajaribu kufanya ninii. . .kila kitu jinsi tunavyopaswa kukifanya, sasa, hatutafanikiwa.

88 Sasa, huyu Melkizedeki, Mfalme wa Salemu, Maliki, Kuhani wa Mungu Aliye Juu, alikutana na Ibrahimu akambariki. Na akampa fungu lake la kumi, Ibrahimu alimpa. Naye alikuwa ni Mfalme wa Salemu. Ndipo akaleta mkate na divai, ushirika, akampa Ibrahimu baada ya vita, baada ya hao watu kushindwa.

89 Sasa, "Vita vyote," kama ninavyosema, "vinapiganwa kwa kanuni." Sasa, kama mna vita ndogo kanisani, lazima iwe ni ya maadili ya kweli. Mnapaswa kuwa mkipigania jambo lililo sahihi. Na kila mshiriki wa kanisa anapaswa kufanya hivyo. Sasa, fundisho hili ni kwa ajili ya kanisa. Hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa hapa. Hiyo ndiyo sababu ninasimama hapa. Hilo ndilo kusudi la Neno la Mungu, ni kwa ajili ya kanisa.

90 Kamwe msiache jambo lo lote lilizuie kanisa hili. Kama likilizuia, mna hatia, kila mmoja wenu. Nanyi, katika makanisa yenu mbali mbali, kama jambo fulani linaenda vibaya kanisani mwenu, ninyi mna hatia, kwa kuwa ninyi ndio mwangalizi wa kanisa hilo. Si kazi ya mchungaji. Si kazi ya halmashauri ya shemasi. Ni juu yako, wewe binafsi, kumwendea ndugu huyo na kuona kama unaweza kumpatanisha. Kama huwezi, basi wachukue wawili ama watatu pamoja nawe, kisha mrudi. Asiposikia hayo; liambie kanisa. Ndipo anafukuzwa kutoka katika Ufalme wa Mungu, Mungu alisema, "Mkimfukuza huko, nitamfukuza Hapa, kama mmepitia katika utaratibu huu." Ndipo atamwachilia Ibilisi awekwe vilivyo. . .kuangamizwa kwa mwili wake. Na ndipo atarudi. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo njia ya kumfanya arudi. Kama yeye ni mwana wa Mungu, atarudi. Kama sivyo alivyo, mbona—mbona, ataendelea, na ndipo Ibilisi atampeleka mahali pake pa Milele.

91 Sasa, kusudi lake. Kama ukimsingizia tu mtu fulani, basi hilo ni jambo lingine. Lakini, kama mtu huyo ana hatia! Naye Lutu alikuwa ameshuka akaenda kule na alikuwa amerudi

nyuma, ingawa alikuwa ni Mwebrania. Alikuwa ameshuka akaenda kule na alikuwa amerudi nyuma. Yeye alikuwa katika neema, bali alikuwa ameanguka toka kwenye neema. Ndipo wakati alipotoka . . . Naye Lutu—Lutu alikuwa ameokoka. Kamwe usifikiri Lutu hakuwa ameokoka. Alikuwa ameokoka. Kwa sababu, wakati wote alipokuwa mahali pabaya, Biblia ilisema, ya kwamba, "Dhambi za Sodoma ziliisumbua nafsi yake yenye haki kila siku." Sasa, mwili wake ulikuwa ukifanya jambo moja. Na mwisho wake ulikuwa ni nini? Alileta aibu zaidi. Mke wake aligeuka akawa nguzo ya chumvi. Alizaa watoto na binti zake. Kwa hiyo, unaweza kuona ni aibu ya jinsi gani jambo hilo lilileta, kwa kuwa alikuwa ameanguka akatoka kwa neema wala hakujirejesha tena kamwe. Ndipo ilibidi Mungu amwondoshe duniani.

92 Lakini, bado, yeye alikuwa ni ndugu aliyeanguka, naye Ibrahimu alifanya yote aliyoweza kumrudisha tena. Nayo Roho iliyokuwa katika Ibrahimu, ni Roho ya Kristo iliyo kanisani siku hizi. Haidhuru ndugu huyo amefanya nini, utafanya yote uwezayo kumrudisha katika ushirika wa Kristo tena. Haidhuru amefanya nini, utajaribu kwa bidii sana.

93 Sasa, tunataka kuangalia hapa tena, tunapoendelea na somo hili la huyu Melkizedeki, Kuhani huyu mkuu wa Salemu, na muumba wa Mbingu na nchi. Sasa, akiwa kwanza:

> *Hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu; huyo adumu kuhani milele.*

Sasa angalia. Yeye hakuwa Mwana wa Mungu. Alikuwa ni Mungu wa Mwana. Hakuwa Mwana wa Mungu, Melkizedeki hakuwa, bali alikuwa ni Baba wa Mwana wa Mungu.

94 Sasa, mwili huu aliokuwa nao, alikuwa ameuumba. Haukuwa umeletwa kupitia kwa mwanamke. Kwa hiyo akiwa na mwili huo ulioumbwa, asingeweza . . . Mwili fulani aliokuwa ameuumba, Yeye Mwenyewe, kusudi ajifunue Mwenyewe.

"Hakuna mtu awezaye kumwona Mungu wakati wo wote. Mungu ni roho." Macho ya kibinadamu hayaoni mambo hayo, isipokuwa iwe ni katika umbo kama la Nguzo ya Moto, ama chochote kile hilo umbo lilichokuwa, ama iwe ni katika umbo la kiumbe fulani walichoona kwa ono. Lakini ninii . . . Mungu hana budi kujifunua kwa njia fulani. Pia Mungu alijifunua Mwenyewe kwa Ibrahimu, katika umbo la mwanadamu. Alijifunua kwa Musa, katika umbo la mwanadamu. Alijifunua kwa wana wa Israeli, katika umbo la Nguzo ya Moto. Alijifunua kwa Yohana Mbatizaji, katika umbo la hua. Unaona, Yeye hujifunua katika sura hizo.

Alipokuwa akijifunua katika sura ya Mtu, kama Mfalme wa Salemu; wa Yerusalemu; si wa Yerusalemu ya duniani, bali

Yerusalemu ya Mbinguni. Yeye alijifunua katika sura hiyo. "Alifananishwa" na Mwana wa Mungu.

95 Sasa, ilimbidi Mwana wa Mungu aje kupitia kwa mwanamke, apate kuumbwa hapa; kwa tumbo la uzazi la mwanamke, kwa maana kupitia katika kitu hicho hicho yalikuja mauti.

96 Naye asingeweza kupitia kwa njia ya maumbile kama Mungu alivyofanya hapo mwanzo. Mungu alipomfanya mtu hapo mwanzo, mwanamke hakuwa na uhusiano wowote na jambo hilo. Mungu alisema tu, "Iwe," ndipo mtu akatoka katika mavumbi. Alimwita, bila ya mwanamke ye yote kuwa na uhusiano wowote na jambo hilo. Lakini, mwanamke, wakati huo sehemu ya mwanamke ilikuwa katika mwanamume.

97 Ndipo Mungu akamtoa mwanamke kutoka katika ubavu wa Adamu. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ndipo mwanamke akaenda akamleta mwanadamu kwa kujuana kimwili. Kwa hiyo njia pekee ambayo Mungu angeweza kufanya... Yeye asingeweza kuja katika theofani hiyo. Asingeweza kuja kama Melkizedeki. Ilibidi aje kama mwanadamu, na ilibidi aje kupitia kwa mwanamke. "Mzao wako utakiponda kichwa cha nyoka, na kichwa chake kitakiponda kisigino chako." Mnalipata? ["Amina."] Ilibidi Mungu aje kupitia kwa mwanamke; Naye alikuja, wakati alipoishi katika mwili Wake wa Mwanawe, Kristo Yesu. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Ndipo aliitoa Damu Yake Mwenyewe kama dhabihu. Kisha akautoa Uhai Wake, ili kwamba kwa njia ya mauti, aweze kukuokoa wewe upate Uzima wa Milele.

98 Kwa hiyo Mungu alikuja basi, Naye "akafananishwa" na Mwana wa Mungu. Unaona? Yeye alikuwa ni Mwanadamu aliyeumbwa kama Mwana wa Mungu. Sasa, Yeye asingekuwa Mwana wa Mungu, kwa kuwa Mtu huyu ni wa Milele.

99 Mwana wa Mungu alikuwa na mwanzo, Yeye alikuwa na mwisho. Alikuwa na wa—wakati wa kuzaliwa Kwake, alikuwa na wakati wa mauti Yake. Alikuwa na mwanzo na mwisho pia. Alikuwa na baba na mama pia.

100 Mtu huyu hakuwa na baba wala mama, mwanzo wala mwisho wa wakati. Bali alifanywa, Mtu huyu, Melkizedeki, aliumbwa kwa mfano *wa* Mwana wa Mungu.

101 Sasa, Mwana wa Mungu, alipokuja ulimwenguni, katika mfano wa mwanamke, kupitia kwa mwanamke, katika mfano wa mwanamume; naye akauawa, akafufuka tena katika siku ya tatu, akafufuka kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu, sasa adumu milele. Na alimradi mwili huo unadumu, sisi nasi tunadumu pia. Na kwa kuwa alifufuka katika mavumbi, sisi nasi tutafufuliwa katika mfano Wake. Hiyo hapo hadithi ya Injili. Jina la Bwana libarikiwe. Si Malaika, si viumbe vya kimbinguni, si kundi la

watu wenye shauri moja, bali ni wanaume na wanawake, amina, watakaosimama katika mfano Wake. Naam, bwana.

102 Kama vile ambavyo mara nyingi nimesimulia jambo hili, ninalisema tena hapa wakati huu. Linaonekana linafaa. Nilikuwa nikichana, hizi nywele kama tano ama sita nilizobakiza. Ndipo mke wangu akasema, "Billy, unakuwa na upara."

103 Nikasema, "Lakini sijapoteza hata moja ya hizo."

104 Akasema, "Ziko wapi?"

105 Nikasema, "Niambie zilikokuwa kabla sijazipata, nitakwambia mahali zinaponingojea." Hiyo ni kweli.

106 Nilikuwa mpi—mpiganaji, mwanandondi. Nilikuwa mwenye nguvu na mkubwa. Nami nilijisikia, kama ungeweka kanisa hili mgongoni mwangu, ningeshuka nitembee barabarani nalo. Nawaambia, ninapoamka kila asubuhi hivi sasa, ninatambua kuna miaka arobaini na kitu imepita. Unaona? Siko jinsi nilivyokuwa. Ninadhoofika, kila siku. Ninapoangalia mikono yangu na kuwazia, "Angalia hapa. Vema, ninakuwa mzee." Ninaangalia mabega yangu. Ninaona nimeongezea uzito mwingi. Nilikuwa nikivaa mkanda wa ishirini na nane. Ninavaa wa thelathini siku hizi. Unaona, ninazeeka, ninanenepa, ninachakaa.

107 Ni kitu gani? Ninakula vitu vile vile nilivyokuwa nikila. Ninaishi msafi na vizuri zaidi kuliko vile nilivyokuwa nikiishi, jambo lile lile. Bali Mungu amenipangia wakati, nami sina budi kuupokea. Lakini wazo lililobarikiwa ni, kwamba, siku hiyo, Yeye atanifufua tena. Na kila kitu nilichokuwa wakati nilipokuwa na umri wa miaka ishirini na mitano, nitakuwa hivyo tena milele. Amina. Haya basi. Ninajali nini uzee? Nitamshinda Ibilisi katika huo kwa miaka na miaka, nikijua jambo hili, ya kwamba ninamwamini Yeye. Kipindi hiki kidogo ni kitu tu kidogo, cha muda mfupi, hata hivyo. Kama tungalidumu tu miaka sabini, umri wa miaka sabini, muda wetu tulioahidiwa, huo—huo ni kitu gani ila ni taabu na huzuni? Ni kitu gani? Je! ungebadilisha nyumba hii ya virusi kwa kitu hicho kitukufu huko ng'ambo?

108 Mbona, Jina la Bwana litukuzwe! Kitu fulani kilichoko ndani yangu kilikutana na na huyo Melkizedeki siku moja, Naye akanitamkia amani na akanipa Uzima wa Milele. Na maisha haya hayana maana yo yote bali ni maskani ya kuhubiria Injili. Ninasema jambo hili kwa uaminifu wote, Biblia hizi mbili zikiwa zimefunguliwa hapa mbele yangu. Kama Mungu wangu alikuwa amemaliza na mimi kuihubiri Injili, wala nisingeweza kumfanyia jambo lo lote zaidi tena, watoto wangu walikuwa wakubwa kujishughulikia, Naye anataka kunichukua sasa hivi, "Amina," hilo latosha. Naam, bwana.

109 Inaleta tofauti gani kama mimi nina umri wa miaka themanini ama kama nina ishirini? Niko hapa tu kwa ajili ya jambo moja: kumtumikia Bwana. Hivyo tu. Kama ningali ninaweza kuihubiri Injili kama ninavyofanya sasa, wakati nina umri wa miaka themanini, inaleta tofauti gani kama nina umri wa miaka arobaini ama themanini? Kuna watu wengi wenye umri wa miaka themanini usiku wa leo. Na kuna watoto wengi watakaokufa, wakati mtu mwenye umri wa miaka themanini ataishi zaidi ya wengi wao. Inaleta tofauti gani? Ni swala ya nia yako, kanuni zako, nasi tuko hapa kumtumikia Bwana Yesu. Hivyo tu.

110 Nikijua jambo hili, ya kwamba, "Maisha haya ni mvuke ambao mwanadamu anazungumzia habari zake; ambao siku moja ulikuwako, halafu hauko." Bali kama tuna Uzima wa Milele, Mungu ameahidi ya kwamba atatufufua tena. Nasi tutakula ushirika pamoja Naye wakati siku zitakapokwisha, na wakati atakaposema, "Ingieni katika furaha za Bwana, mlizoandaliwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu."

111 Basi inaleta tofauti gani hapa, kama tuna cho chote ama hatuna? Kama sisi ni vijana ama kama sisi ni wazee, inaleta tofauti gani? Jambo muhimu, je! uko tayari kumlaki? Je! unampenda? Unaweza kumtumikia? Umeyaacha kabisa mambo ya ulimwengu? Je! umekutana na Melkizedeki tangu vita vilipokwisha?

112 Mungu ahimidiwe! Yapata umri wa miaka ishirini na moja, nilikuwa, na siku moja nilikuwa na vita na *hili*, *lile*, na *lile lingine*. Nisingeweza kuamua kama nilitaka kuwa mwanandondi, ama kama nilitaka kuwa mtegaji, au mwindaji, kile ninachotaka kuwa. Lakini nilikutana na Melkizedeki, Naye akanipa ushirika, na tangu wakati huo lilitatuliwa milele. Haleluya! Nimeenda upande Wake. Nimekuwa nikifurahia njiani. Na wakati inapofikia mwisho wa njia, na mauti yananikazia macho usoni; jinsi ninavyojisikia sasa, kamwe sitayaogopa. Nitatembea, ninataka kutembea nikabiliane nayo, nikijua jambo hili, ya kwamba ninamjua Yeye aliyeahidi, hiyo ni kweli, ya kwamba ninamjua katika nguvu za kufufuka Kwake. Atakapoita kutoka katika wafu, nitatoka miongoni mwao. Hiyo ni kweli, nikimjua katika nguvu za kufufuka Kwake. Inaleta tofauti gani, kama mimi ni mzee ama ni kijana? Kama mimi ni mdogo ama kama mimi ni mkubwa? Kama nimeshiba ama nina njaa? Kama nina mahali pa kulala ama sina?

113 "Ndege wana viota, na mbweha wana tundu, bali Mwana wa Adamu hana mahali pa kulaza kichwa Chake," bali Yeye alikuwa ni Mfalme wa Utukufu.

114 Sisi ni wafalme na makuhani usiku wa leo. Inaleta tofauti gani kama tuna cho chote ama hatuna? Alimradi tu tuna Mungu, sisi ni zaidi ya washindi. Sisi ni zaidi ya washindi.

Tuliketi katika Uwepo wa Mungu, katika ushirika wa Roho Mtakatifu, tukila ushirika wa Kiroho toka katika mikono ya Yeye aliyeshuhudia, "Nilikuwa Yeye aliyekufa, na ni hai tena, Nami ni hai milele." Tukiketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Loo, Jina Lake takatifu litukuzwe. Inaleta tofauti gani?

Hema ama kibanda, nijali nini?
Wananijengea jumba la mfalme Kule!
La rubi na almasi, na fedha na dhahabu,
Makasha Yake yamejaa, Yeye ana utajiri usiotamkika.

115 Nilikutana naye siku moja nilipotoka vitani. Niliweka tunzo zangu chini. Sijapigana vita tangu wakati huo; Yeye ananipigania. Mimi ninatulia tu kwenye ahadi Yake, nikijua jambo hili, ya kwamba ninamjua Yeye katika nguvu za kufufuka Kwake. Hilo ndilo tu lenye umuhimu. Ni kitu gani kingine chenye umuhimu?

116 Tufanye nini? Kwa nini kuwazia kuongeza mkono mmoja kwenye kimo chako? Unajali nini kama nywele zako ni za kipilipili, ama kama una zozote ama huna? Inaleta tofauti gani? Kama wewe ni mzee, kama una mvi, kama umeinama mabega, kama hujainama, inaleta tofauti gani? Amina. Hiki ni kipindi tu, kipindi cha muda mfupi, bali Hayo ni ya milele na milele. Na wakati dahari ya wakati ikiendelea, wakati nyakati zikiendelea, wewe hutabadilika kamwe, na kupitia kwenye nyakati Zake za Milele zisizo na mwisho. Inaleta tofauti gani?

117 Nina furaha sana nilikutana Naye. Nina furaha sana Yeye alinipa ushirika, siku moja, Melkizedeki yeye yule aliyekutana na Ibrahimu akitoka kuwapiga wale wafalme. Hakika. "Mungu wa Mbinguni," yule El Elioni; yule "MIMI NIKO mkuu," si yule nilikuwa; yule MIMI NIKO, wakati uliopo. "Naye akambariki."

118 Sikilizeni hapa mbele kidogo tu, kusudi tupate kuleta hilo somo karibu zaidi pamoja. Sasa kifungu cha 4.

Basi, angalieni jinsi mtu huyo alivyokuwa mkuu, . . .

Ninafikiri hivyo tu, pia. "Angalieni jinsi Mtu huyo alivyokuwa mkuu." Yeye ni zaidi ya Mwana wa Mungu. Mwana wa Mungu alikuwa na baba na mama; Yeye hakuwa nao. Mwana wa Mungu alikuwa na mwanzo wa wakati Wake na mwisho wa wakati Wake; Yeye hakuwa nao. Huyo alikuwa ni nani? Huyo alikuwa ni huyo Baba wa Mwana. Hivyo ndivyo alivyokuwa.

. . .angalieni jinsi mtu huyo alivyokuwa mkuu, hata. . .ambaye Ibrahimu, baba yetu mkuu, alimpa sehemu ya kumi ya nyara zote.

119 Sasa sikilizeni kwa makini.

Na katika wana wa Lawi nao, wale waupatao ukuhani, wana amri kutwaa sehemu ya kumi kwa watu

wao, yaani, ndugu zao, kwa agizo la sheria, ijapokuwa wametoka katika viuno vya Ibrahimu.

120 Sasa angalia jambo hili kama unataka kuona jambo fulani.

Bali yeye, ambaye uzazi wake haukuendelezwa kwa. . .*alitwaa sehemu ya kumi kwa Ibrahimu, akambariki yeye aliye na ile ahadi.*

121 Ibrahimu alikuwa na ile ahadi, naye Mtu huyu alimbariki Ibrahimu aliyekuwa na ile ahadi. Huyu alikuwa ni nani? Wana wa Lawi waliwatolea ndugu zao fungu la kumi ama. . .Ndugu zao waliwatolea fungu la kumi. Walikuwa na amri ya Bwana kuchukua sehemu ya kumi ya yale ndugu zao waliyopata, kwa ajili ya riziki yao, kwa maana walikuwa wao ndio ukuhani. Sasa, hicho ndicho kinachoondoa ukuhani wa Melkizedeki, unaponena habari zake, papo hapo. Hiyo ni kweli. Lakini Mtu huyu. . .Yaani yule aliyekuwa na ahadi, mtu aliye mkuu kuliko wote duniani, Ibrahimu, alikutana na Mtu huyu na akamtolea fungu la kumi. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ilibidi awe mkuu zaidi.

122 Sikilizeni.

Wala haikanushiki kabisa kwamba mdogo hubarikiwa na mkubwa.

Hakika. Angalia kwamba Yeye ni nani.

Na hapa wanadamu wapatikanao na kufa hutwaa sehemu ya kumi;. . .

Huo ni ukuhani wa mfano wa makunani na wahubiri, na kadhalika. Watu wanaopokea fungu la kumi, wanakufa. Unaona?

. . .bali hapa yeye ashuhudiwaye kwamba yu hai.

123 Kwa nini mtu achukue fungu la kumi, kama angalikuwa na ninii. . .kama kamwe hakuzaliwa, wala hatakufa kamwe, na alikuwa tangu mwanzo hata mwisho, wala—wala kamwe hana baba wala mama wala wazazi, na alimiliki Mbingu zote na dunia na yote yaliyomo ndani yake, angepokea fungu la kumi la nini? Kwa nini amtake Ibrahimu atoe fungu la kumi? Unaona ni jambo la lazima jinsi gani kutoa fungu la kumi? Kutoa fungu la kumi ni sawa. Kila Mkristo ana wajibu wa kutoa fungu la kumi. Hiyo ni kweli. Halijabadilika kamwe.

124 Sasa:

Tena inaweza kusemwa ya kuwa, kwa njia ya Ibrahimu, hata Lawi aliyepokea *sehemu ya kumi alitoa sehemu ya kumi.*

125 Sasa, loo, hiki hapa kitu fulani.

Kwa maana alikuwa katika viuno vya baba yake, hapo Melkizedeki alipokutana naye.

126 Ati nini, ati Lawi? Ibrahimu alikuwa babu wa babu wa Lawi. Nayo Biblia ilisema hapa, ya kwamba, “Lawi alitoa fungu la kumi alipokuwa katika viuno vya Ibrahimu.” Vizazi vinne kabla hajakuja duniani, alikuwa akimtolea Melkizedeki fungu la kumi. Jina la Bwana litukuzwe!

127 Kwa hiyo, ninyi ambao hamwezi kuamini katika kuchaguliwa tangu zamani kabla ya kuwekwa kwenye nafasi yako; na hapa, vizazi vinne kabla Lawi kamwe hajatoka katika viuno vya Ibrahimu, alikuwa akimtolea Melkizedeki fungu la kumi. Laiti tungalikuwa na wakati wa kupitia hili katika Maandiko.

128 Kama ukilichukua na kulipeleka kwenye kama Yeremia 1:4, Mungu alisema, “Nilikujua kabla hujafanywa katika tumbo la uzazi la mama yako. Nami nikakutakasa na kukuweka kuwa nabii kwa mataifa.” Basi unaweza kusema ulifanya nini? Ninaweza kusema nilifanya nini? Mungu ndiye alirehemu. Mungu alitujua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

129 Hakutaka kwamba ye yote apotee. Hakika hakutaka. Lakini kama Yeye ni Mungu, Yeye alijua ni nani angeokolewa na ni nani asingeokolewa, la sivyo Yeye hakujua kitu. Kama hakujua . . . Kama hakujua ni nani atakayekuwa kwenye Unyakuo, kabla ulimwengu kamwe haujaumbwa kamwe, basi Yeye si Mungu. Kama Yeye hana kikomo, angeninii . . . Yeye alijua kila kiroboto, kila inzi, kila chawa, kila tekenya, ambaye angekuwa duniani, kabla ulimwengu haujaumbwa. Hiyo ni kweli. Yeye alijua mambo yote. Kabla ya kuweka misingi ya ulimwengu, Yeye alitujua. Biblia ilisema, ya kwamba, “Alitujua na kutuchagua tangu zamani.”

130 Hebu na tulitatue jambo hili mara moja tu. Hebu na turudi katika Waefeso, mlango wa 1. Mlango wa 5 . . . Mlango wa kwanza wa Waefeso, kwa dakika moja tu. Ninataka kusoma hapa kwa dakika moja tu, ili mpate kufahamu kweli kweli ya kwamba si jambo fulani tu ninalojaribu kuwaambia. Ni jambo ambalo Mungu anajaribu kuwaambia. Unaona? Sasa sikilizeni haya, kwa makini sana, mlango wa kwanza wa Waefeso.

> *Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa mapenzi ya Mungu; . . .*

Mtu yule yule aliyeandika waraka wa Waebrania, anauandika waraka huu.

> *. . . kwa watakatifu . . .*

Hii si kwa wasioamini, bali ni kwa watakatifu, waliowekwa wakf- . . . watakatifu.

> *. . . walioko* [Efeso] *wanaomwamini Kristo Yesu.*

> *Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo.*

Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo;. . .

"Kama vile alivyoninii . . . " Sasa, sikilizeni kwa makini sasa, kifungu cha 4.

Kama vile alivyotuchagua sisi katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, . . .

Hawa "sisi" ni akina nani pale? Kanisa.

. . . alituchagua katika yeye (Kristo) *kabla ya kuwekwa misingi, dunia, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo.*

Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi Yake mwenyewe,

131 Ni nani aliyefanya hivyo? Mungu Ndiye aliyefanya hivyo. Mungu alijua tangu mwanzo ni nani angeokolewa na ni nani asingeokolewa. Hakika. Hakuwa anataka kuwa mtu ye yote apotee. Bali Yeye hakumtuma Yesu hapa kuona tu kama unge-—kama ungetenda kama, "Vema, maskini Yesu, namsikitikia. Labda afadhali niokolewe na kuthibitisha jambo hilo." La, bwana.

132 Mungu alijua hapo mwanzo ni nani angeokolewa na ni nani asingeokolewa. Kwa hiyo, basi, Yeye alijua ya kwamba wengine wangeokolewa, kwa hiyo akamtuma Yesu kufanya upatanisho kwa ajili ya wale aliotangulia kuwajua. "Kwa maana hao aliotangulia kuwajua, Yeye aliwaita. Na hao aliowaita, aliwahesabia haki. Na hao aliowahesabia haki, ame- (wakati uliopita) -watukuza." Haya basi.

133 Kwa hiyo si wewe unayejiangalia, ni neema ya Mungu inayokutunza. Hukujiokoa, wala hakuna jambo ulilofanya kustahili kuokolewa. Ni neema ya Mungu iliyokuokoa. Neema ya Mungu ilikuita. Kutangulia kujua kwa Mungu kulikujua. Yeye alijua ya kwamba ungekuwa katika kanisa hili usiku wa leo, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kama Yeye hana kikomo. Kama hana, Yeye si Mungu. Kama alijua mambo yote, Yeye alikuwa ni Mungu. Kama hakujua mambo yote, Yeye hakuwa Mungu. Kama Yeye ni Mwenyezi Mungu, Yeye anaweza kufanya mambo yote. Kama hawezi kufanya mambo yote, Yeye si Mwenyezi Mungu. Haya basi.

134 Kwa hiyo unawezaje kusema ni jambo ambalo ungeweza kufanya? Si jambo lolote unaloweza kufanya. Ni upendo na neema ya Mungu kwako, kwamba wewe hata upo hapa. Hakuna kitu ungaliweza kufanya, Mungu alikuita kwa neema Yake; ukasikiliza, ukasikia, ukakubali.

135 "Vema," unasema, "Ndugu Branham, hilo linafanya mtu afanye atakavyo." Bila shaka linalifanya hivyo. Wewe ni huru.

"Vema, jamaa huyo anaweza kufanya lo lote atakalo." Kabisa. Daima ninafanya ninalotaka kufanya. Bali kama wewe ni Mkristo, hutaki kufanya mabaya.

136 Yule pale maskini msichana mdogo anayeketi kule nyuma usiku wa leo, mke wangu. Ninampenda na yote yaliyo ndani yangu. Nami kama nilijua ya kwamba ningalizurura na mwanamke mwingine na nidanganye, kisha niende nikamwambie, na kusema, "Meda, nilifanya jambo baya," unafikiri ningefanya jambo hilo? Kama ninampenda vilivyo, sitafanya jambo hilo. Hiyo ni kweli.

137 Sasa, vipi kama ningesema, "Loo, siwezi kufanya hivyo. Sababu, nitawaambieni kwa nini. Yeye atanitaliki, nami nina . . . Loo, mimi ni mhubiri. Unaona vile hilo lingefanya? Wataniondoa mimbarani, kama angenitaliki. 'Mwanamume aliyetalikiwa, loo!' Nina watoto watatu. Nisingewazia jambo hilo. Lakini, jamani, mimi . . . "? Vema, kama hivyo ndivyo ilivyo, wewe ungali ni wa kisheria. Sikumwoa kwa msingi wa kisheria. Si msingi wa kisheria unaonifanya niishi mwaminifu kwake. Ni kwa sababu ninampenda. Sishurutiki kufanya jambo lo lote. Ninalifanya kwa hiari yangu kwa sababu ni jambo la mapenzi. Na kama unampenda mke wako, utafanya jambo lilo hilo.

138 Na kama unampenda mke wako namna hiyo, kwa upendo wa *fileo*, unapaswa kufanya nini kwa Kristo na upendo wa *agape*, ambao una nguvu mara milioni moja, kama kweli unampenda Mungu? Kama nilijua usiku wa leo ningeweza nitoke niende na kunywa pombe, kama nilijua usiku wa leo ningezurura na kuwa mzinzi, kama nilijua, usiku wa leo; kama hilo hata lilikuwa liko moyoni mwangu kufanya jambo hilo, nami nikaondoka nikaenda nikalifanya, nikijua ya kwamba atanisamehe, nisingefanya jambo hilo. Ninampenda sana. Ninampenda. Hakika. Bila shaka.

139 Hiyo ndiyo sababu nisingeuza tukio langu kwa madhehebu yoyote, (la, bwana), si Assemblies of God, si kanisa la Mungu, si Piligrim Holiness, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Katoliki. Nisingechukua chochote ambacho kingetolewa, kwa ajili ya tukio hili. Kwa maana, halikuja hata kidogo kwa njia ya mwanadamu. Lilikuja kwa njia ya Mungu. La, bwana. Nisingeuza haki zangu za mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya roki yoyote ya Elvis Presley, ama kwa ajili ya kundi lake la Katoliki, ama Makadilaki, ama dola zake milioni moja, na kadhalika, anazopata kila mwezi. La, bwana. Ninampenda Yeye. Na kama nikininii . . . Mradi tu ninampenda namna hiyo, nitaishi mwaminifu Kwake. Na kama Mungu ameniita na kunichagua, Yeye ameweka kitu fulani ndani yangu, nami ninampenda.

140 Ninamkumbuka Bw. Isler. Nyote mnamjua, karibu ninyi nyote. Yeye amekuja hapa, seneta wa jimbo la Indiana; alikuja hapa, akapiga gita lake. Mtoto wangu alipokufa, mke wangu

alipokufa, na wote wamelala hapa makaburini. Nami nilikuwa nikipanda kwenda barabarani, nimeweka mikono yangu nyuma yangu, nikilia. Yeye aliruka akatoka kwenye lori lake dogo la zamani, akaja akanikumbatia kwa mkono wake, kasema, "Billy, ninataka kukuuliza swali." Kasema, "Nimekusikia ukihubiri mpaka karibu uanguke mimbarani. Nimekusikia pembeni mwa barabara na kila kitu, ukipaza sauti kwa ajili ya Kristo." Kasema, "Sasa Yeye alimchukua baba yako. Alimchukua ndugu yako. Akawanyakua wote wawili, nao walikufa kwenye mikono yako. Hapo akafa. Mke wako alikufa, akiishika mikono yako. Na mtoto wako mchanga alikufa, huku wewe unamwita Yeye akusaidie. Naye akakupa kisogo. Je! unasema nini juu Yake?"

141 Nikasema, "Ninampenda kwa yote yaliyo ndani yangu. Kama akinipeleka kuzimu, bado nitampenda." Yeye ni mwenye haki. Sisemi jambo hilo; miaka ishirini na sita imelithibitisha jambo hilo. Hiyo ni kweli.

142 Kama unampenda! Si swala la jukumu, kwamba, "Siwezi kufanya *hivi*, wala siwezi kufanya *vile*." Unampenda kupita kiasi kutaka kufanya jambo hilo, kwa sababu Yeye amekuchagua. Hukumchagua kamwe. Yeye alikuchagua.

143 Ulisema, "Nilimtafuta Bwana, na kumtafuta Bwana."

"Hakuna mtu anayemtafuta Mungu." Ni Mungu, akimtafuta mwanadamu. Huenda unatafuta kibali Chake, bali Mungu hana budi kubadilisha tabia yako kabla hujaweza hata kumtafuta. Kwa sababu, wewe ni mwenye dhambi, wewe ni nguruwe. Hiyo ni kweli.

144 Na baadhi yenu ninyi watu mnaoenda kanisani na kuishi tu kwa uanachama wenu, mnatoka mnaenda hapa nje na kufanya kila kitu duniani, halafu bado mnarudi na kusema, "Naam, mimi ni mfuasi wa kanisa." Vema hilo liko mbali sana na kuwa wa Mungu. Bila shaka. Mimi sininii . . . Lakini, unaona, watu wanaofanya hivyo, mtu unaweza kujua. Loo, wao ni wafuasi wazuri wa kanisa. Hiyo ni kweli. Unaweza bado uwe mfuasi wa kanisa na ufanye mambo hayo, bali huwezi kuwa Mkristo na kuyafanya.

145 Kama nilivyosema, asubuhi ya leo, "Maskini yule kunguru wa kale, kama kulipata kuwa na mnafiki, ni kunguru." Hiyo ni kweli. Yeye na hua waliketi kwenye safina ile ile, waliketi kwenye kiota kimoja. Naye maskini kunguru aliridhika wakati alipoachiliwa, na akatoka kwenye Kanisa hilo, hata angeweza kwenda huko nje na kuketi kwenye mzoga mmoja uliooza na "koo, koo," na kuula *huu*, na kuula wa farasi, na kuula wa ng'ombe, na wowote ule, aliridhika. Bali Nuhu alipomfungulia hua, asingeweza kupata pumziko kwa ajili ya nyayo za miguu yake. Alikuwa na haki ya kuketi kwenye mzoga wa mnyama kama vile kunguru alivyokuwa nayo, lakini zilikuwa ni tabia

mbili mbalimbali. Mmoja, alikuwa ni hua, kwanza. Yeye alikuwa ni kunguru, kwanza.

146 Lakini, kama ukiangalia, maskini kunguru anaweza kuketi hapa kwenye mzoga uliokufa na kuula, nusu ya siku. Hua ataketi kwenye shamba la ngano na ale, nusu ya siku. Naye kunguru anaweza kuruka moja kwa moja aende huko na kula chakula cha hua, kiasi cho chote atakacho. Angeweza kula kiasi kile kile cha ngano kama kungunguru awezacho . . . ama kama hua awezacho. Lakini yeye, huyo kunguru, anaweza kula chakula cha hua, bali hua hawezi kula chakula cha kunguru. Hiyo ni kweli.

147 Kwa hiyo, maskini mnafiki anaweza kuja kanisani, na kufurahi na kuruka na kumsifu Bwana, na kuendelea namna hiyo, na kurudi moja kwa moja na kufurahia mambo ya ulimwengu. Bali Mkristo aliyezaliwa mara ya pili hawezi kufanya hivyo, kwa sababu upendo wa Mungu unamshurutisha hadi kufikia mahali ambapo hawezi kufanya jambo hilo.

148 Kwa hiyo kama wewe ni Mkristo tu kwa kujiunga na kanisa, na kuacha kufanya jambo *hili* na *lile*, na tamaa ile ile imo ndani yako, unahitaji kutumbukizwa kwingine. Hiyo ni kweli kabisa.

149 Na ninyi wanawake mnaoweza kuvaa hizo ninii ndogo . . . za kaptura, na mtoke moja kwa moja kabisa nje hapa barabarani, na kisha ujiite "mwaminio." Wewe ni mwaminio, bali wewe ni mfano mbaya wa mwaminio, labda. Kama kweli ulikuwa na Kristo moyoni mwako, isingekulazimu kuwazia mambo kama hayo. Sijali hao wanawake wengine wanayofanya, na wasichana wengine wanayofanya, wewe ungekuwa ni wa tofauti, kwa kuwa unampenda Kristo kupita kiasi.

150 Nilizungumza na mwanamke fulani hivi majuzi, katika nyumba fulani, naye akatupa mikono yake juu namna *hii*, kasema, "Kasisi Branham, mimi niko karibu uchi, hapa nyumbani mwangu. Ninazunguka mahali popote."

151 Nikawazia, "Huna haya." Nyumbani kwako mwenyewe, sijali uko wapi. Hiyo ni kweli. Vaa na jiheshimu kama mwanamke, kama bibi anavyopaswa kuvaa. Huna haya. Lakini unaweka . . . Nayo Biblia ilisema, "Ukiyapenda mambo hayo, mambo ya ulimwengu, kumpenda Kristo hata hakumo ndani yako." Na kama unampenda Bwana, kwa moyo wako wote tu, kwa nafsi yako yote, kwa nia yako yote, utavitupilia mbali maskini vitu hivyo vichafu vilivyooza, na vibaya. Hiyo ni kweli.

152 Nawe shemasi, na ninyi wengine hapa, mnaozurura huku mtaani, na kunyosha shingo zenu na kumtumbulia macho kila mmoja wa hao wanawake. Hamna aibu; na ati mnajiita "wana wa Mungu." Ninajua hilo linachoma sana, bali afadhali uchomwe sana kuliko kuteketezwa kwa moto milele kule. Kwa hiyo kama ukifanya mambo hayo . . . Sasa, huwezi kuepuka hilo kama mwanamke akishuka kwenda barabarani, amevaa nusu. Wewe, kama unaangalia, huna budi kumwona, bali unaweza

kugeuza kichwa chako. Biblia ilisema, "Kila amwangaliaye mwanamke kwa kumtamani, umekwisha kuzini naye tayari moyoni mwako."

153 Hebu nikwambie jambo fulani, dada mpendwa, utajibu. Sijali, unaweza ukawa msafi kama yungiyungi. Huenda kamwe hukutenda dhambi ya aina hiyo, dhambi ya uzinzi, maishani mwako. Lakini kama ukivalia namna hiyo, utajibu hukumuni kwa kufanya uzinzi na kila mwanamume aliyekuangalia. Biblia ilisema. Nawe unashuka kwenda mtaani, je! ni nani aliye na hatia, huyo mwanamume? La, bwana. Ni wewe. Ulijianika namna hiyo.

154 Mwanamke ana jukumu kubwa. Ni jukumu takatifu, nzuri, ya ajabu. Bali anapaswa kujiweka hivyo, kushikilia wadhifa wake impasavyo, kama mama, kama mwanamke na ya uanamama. Uanamama unapovunjwa, uti wa mgongo wa taifa lo lote umevunjika. Na hiyo ndiyo sababu, siku hizi, taifa letu limevunjika, ni kwa sababu ya utovu wa uadilifu wa wanawake wetu. Hiyo ni kweli kabisa. Hakika. Ni kuoza miongoni mwetu, ndiko kunakolivunja.

155 Unachohitaji ni kukutana na huyu Melkizedeki wakati mmoja. Amina. Mwache Yeye—mwache Yeye akubariki na akupe divai, ule mkate, Uzima wa Milele. Ndipo utakapoona mambo yako tofauti. Ndipo utaninii. . .Itakuwa ni tofauti. Hutataka vijana wawe wa—wa wakikupigia mbinja ya mbweha, mbinja ya mbwa mwitu, ama chochote kile unachotaka kuiita. La hasha. Utakuwa wa tofauti.

156 Nawe unataka kuniambia ya kwamba unavaa namna hiyo, na kutoka huko nje, kwa kusudi lingine lo lote? Unasema, "Mbona, unajisikia kupoa zaidi." Unadanganya. Si kupoa zaidi. Sayansi inathibitisha ya kwamba si kupoa zaidi. Ni ninii. . . Ni tamaa ya uzinifu iliyokuja juu yako, dada. Hutambui jambo hilo. Sikusudii kukuudhi, ila ninajaribu kukuonya. Wanawake wengi waadilifu, msafi tu awezavyo kuwa, maskini bibi mdogo mzuri, anatoka amevaa vitu hivyo, mtaani, hana habari na kile anachofanya, kwa sababu mhubiri fulani aliyerudi nyuma anahofu mume wako hatatoa fungu lake la kumi kanisani tena. Kama angalipata kukutana na Melkizedeki, asingewazia mambo hayo. Angehubiri Injili. Kama iliwachuna ngozi mgongoni mwao, angeihubiri, kwa vyovyote. Hiyo ni kweli kabisa.

157 Unafanya jambo hilo, na unalifanya kwa sababu roho ya ukware inakuning'inia hapo juu. Na ninyi wanaume ambao mtawaachilia wake zenu wafanye mambo kama hayo, sina imani na ninyi kama mwanamume. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Sasa, hakuna mambo ya kusifusifu juu ya hayo, kwa sababu. . .ama hakuna kuomba radhi. Kwa sababu, hiyo ni kweli. Mtu ye yote atakayemwacha mke wake atoke aende barabarani na kufanya

hivyo, ndugu, unapaswa uwe ukivaa nguo *zake*. Hiyo ni kweli. Wewe, mbona, jamani!

158 Sisemi mke wangu hatafanya hivyo. Lakini itabidi nibadilishwe na kupotoshwa, kutokana na nilivyo sasa, kama kamwe nikiishi naye wakati akiwa anafanya jambo hilo. Na hiyo ni kweli kabisa.

Wasichana wangu, wanaweza wakafanya hivyo watakapofikia kuwa wanawake. Sisemi hawatafanya hivyo. Sijui mimi. Hilo ni juu ya rehema ya Mungu. Natumaini hawatafanya hivyo. Kama wakifanya hivyo, watakanyaga maombi ya baba mwenye haki. Watakanyaga maisha ya mtu fulani aliyejaribu kuishi vema, kama kamwe wakifanya hivyo. Hiyo ni kweli. Lakini ninataka kuishi kiadilifu, kufundisha uadilifu, kuwa mwadilifu, na ningeweza kuwafunza maadili mema. Kama wakifanya jambo hilo, watakazana kuelekea kuzimu, wakiyakanyagia mahubiri yangu, na kumkanyaga Kristo wangu, na kuyakanyaga maonyo yangu, naam, kama wakiwahi kufanya hivyo. Hakika. Hiyo ni kweli.

159 Aibu kwako. Kama utawahi kukutana na Kristo, uso kwa uso, naye akubariki, na kuweka hilo busu la kibali moyoni mwako, pepo wote huko kuzimu hawatakufanya uzivae tena. Hiyo ni kweli. Umebadilika kutoka mautini kuingia Uzimani, na shauku zako zimeelekezwa kwenye mambo yaliyo juu wala si mambo ya dunia. Amina. Afadhali niache somo hilo. Linakera. Vema. Lakini ni Kweli.

160 Vema, tunapoendelea sasa mbele kidogo tu, ndipo tunafunga.

> *. . .katika wana wa Lawi nao, . . .waupatao ukuhani, wana amri kutwaa sehemu ya kumi kwa watu wao, yaani, ndugu zao, kwa agizo la sheria, ijapokuwa* walitoka *katika viuno vya Ibrahimu.*
>
> *Bali yeye, ambaye uzazi wake haukuhesabiwa kuwa umetoka kwa hao, alitwaa sehemu ya kumi kwa Ibrahimu, akambariki yeye aliye na ile ahadi.*
>
> *Wala* inakanushika *kabisa kwamba mdogo hubarikiwa na mkubwa.*
>
> *Na hapa wanadamu wapatikanao na kufa hutwaa sehemu ya kumi; bali* hapa *yeye ashuhudiwaye kwamba yu hai.*

Nami . . .

> *Tena yaweza kusemwa . . ., kwa njia ya Ibrahimu, hata Lawi . . .alipokea fungu la kumi, alipokea sehemu ya kumi, alitoa sehemu ya kumi;*
>
> *Kwa maana alikuwa katika viuno vya baba yake, hapo Melkizedeki alipokutana naye.*

161 Msimamo wa—wako kwa Kristo utakuwa na ushawishi mkubwa sana juu ya vile watoto wako watakavyokuwa. Maisha yako unayoishi mbele ya familia yako yatakuwa na ushawishi juu ya vile watoto wako watakavyokuwa. Maana, Biblia ilisema, ya kwamba, "Atawapatiliza wana maovu ya baba zao hata kizazi cha tatu na cha nne."

162 Sasa, dakika chache tu, kabla ya kufunga.

> Basi *kama ukamilifu* (huo hapo ukamilifu wako tena) *ulikuwapo kwa ukuhani wa Lawi; (maana watu wale waliipata sheria kwa huo); kulikuwa na haja gani tena* kuje. . .*ya kuhani mwingine ainuke, kwa mfano wa Melkizedeki, wala asihesabiwe kwa mfano wa Haruni?*

163 Torati, mshika sheria, unaona, "Loo, inakupasa kufanya jambo *hili*. Usipofanya jambo *hili*, wewe si Mkristo. Kama hushiki sabato! Kama huninii. . .Kama ukila nyama! Kama ukifanya mambo *haya*!" Mawazo haya yote ya kisheria. "Na ni lazima uende kanisani. Usipoenda, utalipa faini kwa hilo. Huna budi kufanya novena." Kitu hicho ni upuuzi. Unaokolewa kwa neema ya Mungu, kwa kujua mbele kwa Mungu, kwa kukusudia Kwake tangu zamani. Mungu alimwita Ibrahimu kwa kumchagua tangu zamani, kwa kutangulia kumjua. Yeye alimwita. Alimchukia Esau, na akampenda Yakobo, kabla ya ye yote wao hajazaliwa. Hiyo ni kweli. Ni—ni kutangulia kujua kwa Mungu kunakojua mambo haya.

164 Unasema basi, "Kuna manufaa gani kuhubiri Injili?"

165 Sasa nitawaambia, jambo hili. Paulo alijibu hilo, ama Yesu alijibu, hasa. Huyu hapa Yesu. Yeye alisema, "Ufalme wa Mbinguni ni kama mtu aliyeenda kwenye hiki, ki—kidimbwi ama ziwa, naye akatupa jarife ndani. Akalivuta. Kutoka mle, alipata kobe. Alipata kasa. Alipata nyoka. Alikuwa na mijusi. Alikuwa na vyura. Alikuwa na buibui. Alikuwa na wala mizoga. Alipata—alipata samaki." Sasa, mtu huyo alikuwa tu akivua.

166 Hiyo ni kama Injili. Hii hapa sasa, ninahubiri Injili. Ninatupa tu jarife. Ninaivuta, ninasema, "Wote watakao, yeyote, na aje." Hawa hapa wengine wakaja, madhabahuni. Wote wanazunguka madhabahu. Wanaomba. Wanalia. Sijui nani ni nani. Si kazi yangu. Sikutumwa kuhukumu.

167 Lakini, kuna wengine mle ndani ambao ni vyura. Kuna wengine ambao ni mijusi. Kuna wengine ambao ni nyoka. Ni, wengine, ni kobe. Na kuna wengine ambao ni samaki. Si kazi yangu kuhukumu. Ninasema, "Baba, hawa ndio niliowavuta."

168 Lakini, chura alikuwa ni chura, tangu mwanzo.

169 Buibui, maskini buibui ataketi pale na kuangalia kila mahali, kitambo kidogo, ayafingirishe hayo macho makubwa, aangalie kila mahali, aseme, "Unajua nini? Mambo haya

nimepata ya kutosha siwezi nikavumilia mengine." Plup, plup, plup, plup, haoo wanatoka nje.

170 Maskini bibi nyoka atainua kichwa chake, na kusema, "Vema, unajua nini? Kama watahubiri hivyo, dhidi ya kuvaa kaptura na kadhalika, hilo linanijumlisha na mimi. Kwa hiyo nitaachana na kundi hilo la watakatifu wanaojifingirisha. Hivyo ndivyo tu walivyokuwa." Wewe ulikuwa ni nyoka tangu mwanzo. Hiyo ni kweli kabisa. Naam.

171 Na huyu hapa maskini bwana chura, akiwa na ule msokoto mkubwa mno mdomoni mwake, kama maksai wa Texas aliyeng'olewa pembe, atasimama pale na kuangalia huku na huko, aseme, "Vema, kamwe haijanihukumu kuvuta sigara. Nitatoka tu kwenye kitu hiki, sasa hivi." Vema, ewe maskini chura wa kale, ulikuwa hivyo, tangu mwanzo. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni kweli kabisa.

172 Tabia yako inathibitisha kwamba wewe ni nani. Maisha yako yanaonyesha, yanaakisi jinsi ulivyo, na vile ulivyokuwa hapo mwanzo. Si vigumu kwangu kuona jambo hilo. Si vigumu kwako kuliona.

173 Kama nilitoka nikaenda kwa Roy Slaughter mkulima anayeketi hapa, nami nikawaona nguruwe huko kwenye lundo la samadi, wakila samadi, sitajisikia vibaya kuhusu jambo hilo. Yeye ni nguruwe. Lakini kama ningalimwona mwana-kondoo juu ya lundo hilo la samadi, ningeshangaa. A-ha. Unaona? Usiwe na hofu, hutamwona pale. Asingeweza kabisa kuivumilia. Hiyo ni kweli.

174 Na mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu anachukia mambo ya ulimwengu. Hiyo ni kweli, "Kwa kuwa ukiipenda dunia au mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako."

175 Kama nikizurura na wanawake kila siku, na kisha nirudi nyumbani, nimwambie mke wangu kwamba nilimpenda, yeye angejua kwamba mimi nilikuwa mwongo. Matendo yangu yangenena kwa sauti kubwa zaidi kuliko maneno yangu. Hakika. Ninamthibitishia ya kwamba sikumpenda, kwa sababu sikuwa mwaminifu kwake.

176 Kama angaliniambia ananipenda, na kila wakati nikiwa sipo, angetoka na mwanamume mwingine, ingethibitisha ya kwamba hakunipenda. Kweli. Matendo yake yanathibitisha jambo hilo. Sijali angejaribu kuniambia kiasi gani, "Bill, ninakupenda, wala hakuna mtu mwingine duniani ila wewe," ningejua alikuwa mwongo.

177 Na unapojaribu kusema, "Bwana, ninakupenda," na unaishi katika mambo ya ulimwengu, Mungu anajua kwanza kabisa, wewe ni mwongo. Kwa hiyo ni kwa nini? Ya nini kukubali tukio la nusu-nusu, na kitu kingine kama hicho, wakati anga kuu za Mbinguni zimejaa jambo lililo halisi? Kwa nini unataka kuwa

Mkristo mnyonge, wa kujifanya, nusu-nusu, usiye na busara? Wakati, unaweza kuwa mtoto halisi wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili, huku kengele za furaha za Mbinguni zikilia moyoni mwako, ukifurahi, na kumsifu Mungu, na ukiishi maisha ya ushindi kwa Yesu Kristo.

178 Sio kujaribu kufanya jambo hilo wewe mwenyewe, kwa sababu utashindwa, kwanza. Lakini mchukue Yeye, ni swala la Neno Lake, na utulie kwenye yale aliyosema yalikuwa ni Kweli. Na umwamini, na umpende, Naye atafanya kila kitu kifanyike kinaganaga vizuri kwako. Jambo ndilo hilo. Wazo ndilo hilo.

179 Basi Bwana awabariki. Sitaki kuwakemea, lakini, ndugu, ni vizuri kabisa kupata karipio dogo. Ninyi ni watoto wangu wachanga. Mnaona? Na baba yeyote anayewapenda watoto wake bila shaka atawarudi, la sivyo yeye si baba mzuri. Je! ni kweli? Hilo ni kweli. Na baba huyu ana kanuni moja tu, na hiyo ni kanuni ya nyumbani. Na Mungu ana kanuni moja tu, na hiyo ni Neno Lake.

180 Kama tunaamini Neno Lake, basi tutaishi kwa Neno Lake. Ni wajibu wetu, kama tulipata kukutana na Mungu. Si kwa sababu unasema, "Vema, ninaenda kanisani, nami sina budi kufanya jambo *hili*." Wewe ni maskini. Usifanye hivyo. Kwa nini unataka kuwa kunguru mwenye mashaka, mdhaifu, mwovu anayejitweza, wakati ungeweza kuwa hua? Hakika. Inakupasa tu ubadilishwe tabia yako. Na unabadilika tabia yako, uwe mwana na binti wa Mungu, uwe na amani na Mungu.

181 Yesu! "Kwa ajili hii Yesu Naye, ili awatakase watu kwa Damu Yake Mwenyewe, aliteswa nje ya malango," Waebrania 13:12 na 13. Warumi 5:1, "Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani," si kwa kupeana mikono, si kwa ubatizo wa maji, si kwa kuwekea mikono, si kwa kupaaza sauti, si kwa kunena kwa lugha, si kwa mhemko wowote. "Bali tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, tuna imani kwa Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo." Tumepita toka mautini kuingia Uzimani, na tumekuwa viumbe vipya, kwa sababu tumemwamini Mwana wa pekee wa Mungu, na kumkubali Yeye kama Mwokozi wetu binafsi. Na Damu Yake inatenda kazi, usiku wa leo, kama upatanisho kwa ajili ya dhambi yetu, kusimama mahali petu.

182 Katika Agano la Kale, kuna mahali pamoja tu pa kuwa na ushirika, hapo ni chini ya damu. Kila mwaminio ilibidi aje chini ya damu. Wakati yule ndama mwekundu alipochinjwa, alifanywa toleo la dhambi. Hana budi kuwa mwekundu. Na katika mlango wa 19 wa Kutoka, kama yeyote wenu angetaka kuusoma. Naye hana budi kuchukuliwa, kwato, vyote, vinateketezwa pamoja kwa moto. Ndipo huyo alifanywa kuwa maji ya utengano. Aliwekwa nje ya malango. Ilibidi ashikwe na mkono ulio msafi. Damu ya ndama huyu ilitangulia . . . kwenye kusanyiko, na kupakwa mara saba juu ya mlango. Na sasa,

kila mtu aliyetiwa unajisi anayeenda pale, hana budi kwanza kutambua na kuona hiyo damu, na kutambua ya kwamba ushirika upo pekee chini ya hiyo damu. Hapo ndipo mahali pekee ambapo mwabudu angeweza kweli kuabudu rasmi, ilikuwa ni chini ya hiyo damu.

183 Ndipo, jambo la kwanza lililombidi kufanya, kabla hajaweza kuja chini ya damu, ilibidi kuweko na haya maji ya utengano aliyonyunyiziwa, na aliye mchafu alitakaswa.

184 Ndipo walichukua maji ya utengano na kumnyunyizia nayo msafiri, na kumtenga na dhambi yake. Ndipo akatembea chini ya hii milia saba ya damu, naye akawa na ushirika pamoja na waamini wengine Mbele za Mungu.

185 Kuna njia moja tu ya kufanya jambo hilo. Si kupeana mikono, si kujiunga na kanisa, si kwa mabatizo, si kwa mihemuko; bali ni kwenda kwenye maji ya utengano, uweke mikono yako, kwa imani, juu ya kichwa cha Yesu, na kusema, "Mimi ni mwenye dhambi, Nawe ulikufa mahali pangu. Na kitu fulani ndani yangu kinaniambia ya kwamba utanisamehe dhambi zangu, nami ninakukubali kama Mwokozi wangu binafsi sasa." Unatembea chini ya Damu, kule, na kufanya ushirika na watoto wa Mungu. Jambo ndilo hilo. Ule mkate, unywe divai, na ufanye ushirika pamoja na kanisa.

186 Loo, Yeye si ni wa ajabu? Yeye si ni mwema? Sasa, hili linaweza kuonekana ni geni kwako, ewe rafiki. Lakini na—nasimama hapa na kusema mambo haya kwa nini? Je! ningeyasema kujaribu kujifanya tofauti na mtu mwingine? Kama nikifanya hivyo, basi ninapaswa kutubu. Ninasema jambo Hilo kwa sababu Mungu alilisema, kwa sababu ni Neno la Mungu. Na sikilizeni. Wakati unakuja, na sasa upo, ambapo watu wataenda kutoka mashariki kwenda magharibi, wakijaribu kupata Neno la Mungu, wala hawawezi kulipata.

187 Unapoingia mkutanoni, jambo la kwanza unalofanya, unaingia mle na unakuta lundo la lugha na fasiri zake, na mtu fulani anainuka na kuendelea kuyanukuu Maandiko; na hicho ni kimwili. Kabisa. Mungu alitwambia "msipayuke-payuke," vipi kumhusu Yeye! Kama ameliandika Hilo mara moja, liamini. Haimlazimu kulisema tena. Lugha na fasiri ni sawa, lakini hayo yanapaswa kuwa ni ujumbe wa moja kwa moja kwa kanisa na kwa mtu fulani, si kimwili tu na vitu kama hivyo. Na ndipo mwendelee katika mambo haya mengine yote.

188 Hapa hivi majuzi, watu wawili walienda kwenye . . . na mtu mmoja na mkewe, na mtu mwingine na mkewe, wamefunga ndoa tu karibuni, walienda wakaingia mahali fulani, wapate kwenda Afrika kama wamishenari. Mtu fulani alisimama na kutoa unabii, na kutoa lugha na fasiri zake, ati, "Kila mmoja alikuwa na mke wa mwingine." Ati, "Haipaswi kuwa hivyo. Walioa kimakosa." Ndipo watu hao wawili walitengana na wake

zao na kuoa tena, mara nyingine tena. Mwanamume mmoja akachukua mke wa huyo mwingine, na huyo mwingine, akafanya vivyo hivyo katika madhehebu mashuhuri ya Kipentekoste, kisha wakaenda Afrika kama wamishenari.

189 Ndugu, unapoweka nadhiri yako, unawajibika kwa nadhiri hiyo mpaka mauti yatakapokuweka huru. Kweli kabisa. Hakika. Unapoweka nadhiri yako, inakufunga.

190 Hayo yote, upuuzi! Na imefikia mahali ambapo unapoenda makanisani, ama ni baridi sana na ya kawaida na yamekauka, mpaka kipimo cha joto la kiroho kitafikia hamsini chini ya sufuri. Watu wanaketi tu kama dutu kwenye achali, wamechacha na hawajali na wamekunjamana. Na kama ukimsikia mtu fulani, huko nyuma kabisa kwenye kona, huenda akaguna "amina" kidogo, mara moja moja, kana kwamba inawaudhi, wote watanyosha shingo zao kama bata mzinga, kuangalia pande zote, waone ni kitu gani kilitukia. Mnajua hiyo ni kweli. Sisemi jambo hilo kwa mzaha. Hapa si mahali pa mzaha. Hiyo ni Kweli. Kweli. Ninasema jambo hilo kwa sababu ni Kweli ya Injili.

191 Na upande huo mwingine, unapata tita la upuuzi wa makelele chungu zima ya mihemuko ya kimwili, na Neno la Kweli la Mungu hatimaye limefikia mahali ambapo ni vigumu kulisikia: ile Injili ya kale ya katikati ya njia, Nuru njiani mwangu, haleluya, Damu ya Mwana-Kondoo, upendo wa Mungu unaotutenganisha na mambo ya ulimwengu.

192 "Je, umenena kwa lugha, ndugu? Hunaye. Je! ulipiga makelele mpaka ukasikia hisi baridi ikipitia mgongoni mwako? Je! uliona mipira ya moto?" Loo, upuuzi! Hakuna kitu kama hicho.

193 Je! umemwamini Bwana Yesu Kristo na kumkubali kama Mwokozi wako binafsi? Na Roho wa Mungu anashuhudia pamoja na roho yako, ya kwamba ninyi ni wana na binti za Mungu. Na maisha yako yanazaa tunda la upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, upole, utu wema. Basi wewe ni Mkristo. Kama hayazai matunda hayo, sijali unafanya nini.

Paulo alisema, "Ningeweza kuutoa mwili wangu uchomwe moto kama dhabihu. Nilijua siri zote za Mungu. Ninaweza kuhamisha milima kwa imani yangu. Ninaweza kunena kwa lugha kama wanadamu na Malaika. Si kitu mimi." Na hayo je? Wakorintho wa Kwanza 13; chunguza kama hiyo ni kweli ama si kweli.

194 Sasa chunguza kama—kama Wakorintho, Wakorintho wa Pili 13, ninaamini ndipo. Ama, vema, ama ni Wakorintho wa Kwanza ama wa Pili. Wakorintho wa Kwanza pale, Wakorintho wa Kwanza 13, ni sawa. "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na Malaika, namna zote mbili zinazoweza kufasiriwa na

zile zisizoweza kufasiriwa, si kitu mimi." Kwa hiyo ya nini kujipumbaza nayo, basi?

195 "Nijapofahamu siri zote za Mungu." Mbona unaenda seminari na kujaribu kusoma kuhusu mambo mengi? Afadhali ujiweke sawa na Mungu, kwanza. Hakika. "Nijaponinii, 'Loo, haleluya iliyobarikiwa!'"

196 Mtu unakuwa hivi kwamba usingeweza kuwa na kusanyiko lolote la watu usipokuwa na mkutano wa uponyaji ama namna fulani za miujiza ikiendelea. "Kizazi kidhaifu na cha zinaa hutafuta vitu kama hivyo." Unaitakia nini hiyo?

197 Paulo alisema angeweza kufanya mambo ya kila namna, hata kuihamisha milima, na hata bado yeye angali si kitu. "Zikiwako lugha, zitakoma. Yakiwapo maarifa, yatabatilika. Ukiwapo unabii, utabatilika. Lakini ijapo ile iliyo kamili, itadumu milele," na upendo ni ukamilifu. "Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee." Ili, "Kila atetemekaye, kila atikisikaye, kila anenaye, kila"? "Kila amwaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa Milele." Aminini jambo hilo, enyi watoto.

198 Wanajaribu kulifanya gumu sana, mambo *haya* na mambo *yale*. Wakati, kwa jumla ni jambo moja: imani yako ya kibinafsi katika Mungu. Hilo ndilo litakiwalo. Hilo linaelezea linavyotakiwa. "Kwa maana kwa imani," si kwa kuhisi. "Kwa imani," si kwa mhemuko. "Kwa imani," si kwa msisimko. "Bali kwa imani," mmeokolewa; na hiyo ni kwa njia . . . " Ati kwa kuwa ulimtafuta Bwana? Kwa sababu ulikuwa u mtu mzuri? Kwa sababu, "Mungu, kwa neema, alikujua tangu zamani na alikuchagua upate Uzima wa Milele."

199 Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote wanijiao mimi, nitampa Uzima wa Milele. Hakuna mtu awezaye kuwatoa katika mkono Wangu. Hao ni wangu. Wameokolewa milele. Ninao. Hakuna mtu awezaye kuwatoa katika mkono wa Baba Yangu, Naye Ndiye aliyenipa hao. Hao ni tunu Zangu za upendo."

200 "Na wote aliotangulia kuwajua, Yeye aliwaita." Yeye hamwiti mtu ye yote isipokuwa alitangulia kumjua. "Wote aliowaita, aliwahesabia haki; wote aliowahesabia haki, aliwatukuza." Kwa hiyo, unaona, tuko kwenye raha kamilifu.

201 Sasa, ninajua kuna watu wengi sana washikao sheria hapa, asilimia tisini yenu. Lakini, angalia, kama mkipenda hebu chukueni tu Hili na mtambue ya kwamba mimi sijaribu kuwaambieni jambo fulani.

202 Ndipo mnasema, "Vema, Ndugu Branham, daima nimefikiria kwamba ilinibidi nifanye *hili* na ilinibidi nifanye *lile*." Kuna tofauti ku—kubwa kwake, ndugu, yale yanayokupasa kufanya na yale unayotaka kufanya. Wewe umeokoka, si kwa sababu ulihusika na kutenda jambo lolote. Umeokoka kwa

kuwa kwamba Mungu alikuokoa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

203 Sikilizeni. Sikilizeni hapa. Biblia ilisema, katika Ufunuo. Nitawachukua kutoka hapo mwanzo hadi cha mwisho sasa. Biblia ilisema, katika Ufunuo, ya kwamba, wakati yule mnyama alipokuja, aliwadanganya wote juu ya nchi. Yule mnyama aliwadanganya. "Aliwadanganya wote walio juu ya nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo . . . " Tangu ufufuo ulipoanza? Je! hilo linasikika kuwa sawa? Vema, tangu yule mhubiri alipohubiri somo hilo lenye nguvu sana? Tangu mtu yule alipoponywa? " . . . tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu."

204 Je! Yesu alichinjwa wapi, huko Kalvari? La, bwana. Yesu alichianjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. "Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu, aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Mungu, hapo mwanzo, wakati alipoiona hiyo dhambi, alipoona kile ambacho kingetukia, Yeye alinena Neno. Naye Yesu alichinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na kila mtu aliyeokoka, aliokoka kulingana na Biblia, wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa katika nia ya Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kwa hiyo wewe ulihesabiwa katika wokovu wakati huo. Kwa hiyo utafanya nini juu ya jambo hilo?

205 Ni Mungu. Jina la Bwana litukuzwe! "Mungu ndiye anayefanya kazi; si katika uwezo wa yeye atakaye wala yeye apigaye mbio, bali ni Mungu arehemuye."

Kama Yesu alichinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ilichukua miaka elfu nne kabla jambo hilo halijatukia katika urahisi. Lakini wakati Mungu alipolinena hapa nyuma, kila Neno la Mungu ni imara. Halikubadilika. Haiwezekani. Haliwezi kushindwa. Na wakati Mungu alipomchinja Mwanawe kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Yeye alikuwa amechinjwa wakati huo kabisa kama alivyokuwa amechinjwa pale Kalvari. Ni kazi iliyomalizika, wakati Mungu anapomtaka hivyo. Pia kumbuka, wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa, wokovu wako ulihesabiwa katika hiyo dhabihu, kwa maana Biblia ilisema ya kwamba jina lako lilikuwa "Limeandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu."

Na hilo je? Basi tutafanya nini? Mungu Ndiye arehemuye. Mungu Ndiye aliyekuita. Mungu Ndiye aliyekuchagua katika Kristo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yesu alisema, "Ha—hamkunichagua kabisa. Mimi niliwachagua. Nami niliwajua, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Haya basi.

206 Kwa hiyo, unaona, hilo linaondoa hofu ndani yako. "Loo, sijui kama ningeweza kudumu kushikilia? Nitafaulu, Mungu

atukuzwe, kama nitaendelea tu kushikilia." Si iwapo kama ninashikilia, ama sitashikilia. Ni iwapo kama Yeye alishikilia, ama hakushikilia. Ni yale—yale aliyofanya, si yale niliyofanya. Ni yale aliyofanya.

Je! liko chini ya sheria ya ukombozi? Hili ni jambo dogo ninalotaka kusema kabla sijafunga.

207 Vipi kama farasi jike angalizaa kitoto cha nyumbu? Na masikio yote mawili ya maskini nyumbu huyo yamechanika. Alikuwa na makengeza, na mwenye magobwe, mwenye mategе. Mkia wake umesimama wima hewani. Ni mnyama wa kutisha jinsi gani! Mbona, mtu yeyote. . .Kama maskini nyumbu huyo angaliweza kuwazia, aseme, "Sasa, ngoja kidogo. Watakapotoka nyumbani asubuhi ya leo, ninawaambia, bila shaka nitapigwa kichwani. Kwa sababu, hawanilishi hata kidogo. Angalia jinsi nilivyo kitu cha kuchukiza. Hata sina nafasi."

208 Vema, hiyo ni kweli. Huna nafasi. "Vema, nilizaliwa katika ulimwengu huu, bali angalia hapa jinsi nilivyo kitu cha kuchukiza. Kwa hiyo ni—ni—ni. . .Kamwe sitapata nafasi. Sitafaulu. Siwezi kufaulu." Unaona?

209 Lakini vipi kama mama yake amefunzwa sheria vizuri? Atasema, "Mwanangu, hiyo ni kweli. Wewe una sura mbaya sana, na hata hufai kula chakula kutoka ardhini. Hiyo ni kweli. Hufai. Lakini, mwanangu, kwa vyo vyote vile, wewe ndiye kifungua mimba changu. Na, unajua, umezaliwa chini ya haki ya mzaliwa wa kwanza. Wala kuhani hatakuona kamwe. Lakini, kuhusu jina lako, hapana budi kuweko na mwana-kondoo asiye na hatia, asiye na dosari, hana budi kufa mahali pako, upate kuishi."

210 Vema, maskini hicho kitoto cha nyumbu kingeweza tu kutupa mateke yake juu na kishangilie. Haileti tofauti yo yote jinsi alivyo, kwa sababu hataonwa na hakimu kamwe, kuhani. Mwana-kondoo ndiye ambaye kuhani humwangalia. Si nyumbu; mwana-kondoo!

211 Na Kristo Ndiye ambaye Mungu humwangalia, si wewe. Ni Kristo. Kwa hiyo kama hana kosa lolote, kunawezaje kuweko na kosa? Anawezaje kupata kosa, wakati wewe umekufa na uhai wako yamefichwa katika Kristo kwa njia ya Mungu, umetiwa muhuri na Roho Mtakatifu? "Wale waliozaliwa na Mungu hawatendi dhambi kwa maana hawezi kutenda dhambi." Anawezaje kutenda dhambi wakati dhabihu kamilifu imewekwa mahali pake? Mungu kamwe haniangalii mimi, Yeye humwangalia Kristo, kwa kuwa sisi tumo ndani ya Kristo.

212 Sasa, kama ninampenda Kristo, nitaishi pamoja Naye. Kamwe Yeye asingeniingiza ndani Yake kama asingejua. Kama Mungu angaliniokoa leo, akijua ya kwamba atanipoteza majuma sita toka leo, Yeye anazuia kusudi Lake. Kweli. Hata hajui ya usoni basi, kama aliniokoa, akijua. Anataka kuniokoa

kwa kusudi gani, akijua atanipoteza? Mungu hafanyi mambo, kisha aghairi mnamo majuma mawili, kutimiza ahadi Yake. Anapokuokoa, hiyo ni kwa wakati na Umilele.

213 Sasa, unaweza kuwa umechochewa, na kusema, "Loo, naam, Mungu atukuzwe! Haleluya! Nilinena kwa lugha. Nilipaaza sauti. Ninaye. Haleluya!" Hiyo haimaanishi unaye. Lakini, ndugu, wakati kitu fulani kinapokuja hapa *chini*, na unatia nanga pamoja na Kristo, ndipo matunda ya Roho yanakufuata. Tunashuhudia, roho yetu pamoja na Roho Wake, ya kwamba sisi ni wana na binti za Mungu. Tafadhalini mpateni Huyo, enyi marafiki.

214 Nitawaweka hapa usiku kucha, nikizungumzia jambo hilo. Ninalipenda. Ninawapenda. Ninarudi kwenye maskani hii ndogo, wakati baada ya wakati, kama Mungu atayahurumia maisha yangu. Ninataka kuwaona mmethibitishwa na kuimarishwa katika Imani hiyo takatifu. Sitaki kuwaona mkirushwarushwa huku na huko, na kila upepo wa fundisho linalopitia hapa, na kuwatikisa, na kupiga makelele, na kuwa na damu kidogo mikononi mwao, ama ukungu kidogo usoni mwao, ama kitu kama hicho, na kuona namna fulani ya—ya—ya nuru mbele yao, na namna fulani ya—ya kitu cha kichoyo, kama Biblia ilivyosema, "Mwenye majivuno moyoni mwake, wala hajaona kitu." Hiyo ni kweli. Ninawatakeni mwe imara katika Neno. Kama ni BWANA ASEMA HIVI, dumuni Nalo, ishini Nalo. Hilo ndilo Urimu Thumimu ya siku hii. Mungu anawatakeni mwishi kwa Hilo. Kama halimo katika Neno, basi lisahau. Mwishie Mungu, mwishie Kristo.

215 Na kama moyo wako ukianza kupoteza njia, unajua kuna jambo fulani lililotukia, rudi madhahabuni na useme, "Kristo, ifanye upya ninii yangu. . . furaha ya wokovu wangu. Nipe ule upendo niliokuwa nao wakati mmoja. Unavuja, Bwana. Kuna kitu fulani nimefanya. Nifanye mtakatifu tena, nisimame. Ee Bwana, hakuna kitu ningaliweza kufanya. Siwezi kuacha *hili* na kuacha *lile*. Ninakutazamia Wewe kulitoa ndani yangu, Bwana, nami ninakupenda."

216 Kisha uondoke kutoka kwenye madhabahu hiyo, mtu mpya katika Kristo Yesu. Ndipo haitakubidi kulitegemea kanisa lako, kumtegemea kuhani wako, kumtegemea mchungaji wako. Unategemea Damu iliyomwagwa ya Bwana Yesu. "Kwa neema mmeokolewa."

Na tuombe.

217 Bwana, mafundisho yenye nguvu namna hii! Wakati umewadia kwa kanisa hili kula chakula kigumu, wala si maziwa ya Neno tena. Tumekaa sana kwenye maziwa sasa, tukimnyonyesha mtoto mchanga chupa yake. Lakini tunapaswa kula chakula kigumu, kwa kuwa ile siku inakaribia. Nyakati kubwa za hatari zimekaribia, na shida nyingi ziko njiani. Nasi

tunajua ya kwamba kamwe hakutakuwako na nyakati nzuri zaidi. Tunajua ya kwamba tuko mwisho. Nyakati zitandelea kuwa mbaya zaidi na zaidi mpaka Yesu atakapokuja, kulingana na Maandiko.

218 Hatuwezi kuwaahidi kitu cho chote katika maisha haya. Bali katika maisha yajayo, tunaweza kuwaahidi hao watu Uzima wa Milele katika Neno Lako, kama watamwamini Mwana wa Mungu na kumkubali kama mpatanishi wao, kama Yeye aliyesimama mahali pao, kama Yeye aliyeziondoa dhambi zao. Tujalie sasa.

219 Jalia wasioamini wawe waamini. Jalia wanaokiri kanisa, hapa usiku wa leo, ambao wamekiri dini na wanaishi tu kanisani, jalia wapokee Tukio na Mungu; hivi kwamba upendo mkubwa sana utaingia moyoni mwao, hata watalia kwa ajili ya dhambi zao, wajifie nafsi zao, na wazaliwe upya na Roho Mtakatifu, na wakiwa wapole na wema, wakiwa wamejaa upendo, na wamejaa furaha na baraka. Wakiishi maisha mazuri sana, mpaka wakolee munyu sana hivi kwamba watafanya watu walio karibu nao, wapate kiu ya kuwa kama wao. Tujalie hayo, Bwana, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake.

Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

220 Sijui, usiku wa leo, kama kungekuwako na mmoja hapa, atakayesema, "Ndugu Branham, kama niliwekwa kwenye mizani ya Mungu wakati huo, kamwe, kamwe, kamwe nisingeweza kupata hizo sifa unazozungumzia usiku wa leo. Ninataka unikumbuke katika maombi, ya kwamba nitabadilisha njia zangu, na Mungu atakuja na kuingia na kuondoa upuuzi huu kutoka kwangu na kunifanya Mkristo halisi"? Je! waweza kuinua mkono wako kwa ajili ya maombi, u—ungependa? Mungu akubariki. Mungu akubariki, Mungu akubariki huko nyuma. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, ndugu mkubwa. Mungu akubariki dada.

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana
  Mungu wa majeshi.
Mbingu na nchi zimejaa Wewe,
Mbingu na nchi zinakusifu Wewe,
Ee Bwana Uliye Juu Sana.

221 "Mtakatifu." Wakati mkifikiria sasa, mkiomba, mnapojisikia mmeshawishika ya kwamba mmekosea, nanyi mnataka kuwa sawa, je! unaweza tu kuinua mkono wako, ukisema, "Mungu, nifanye kile ninachopaswa kuwa"? Mungu akubariki, bibi mdogo. "Mungu, nifanye vile ninavyopaswa kuwa." Mungu akubariki, ndugu, dada, wewe, wewe, wewe *hapa*.

222 Siku inaisha. Ninajua ni vigumu, enyi marafiki, bali ni bora mjue Ukweli sasa. Sasa ombeni kimya kimya.

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu Bwana
Mungu . . .

Yeye ni mtakatifu, peke Yake.

. . . zimejaa Wewe,
Mbingu na nchi zinakusifu Wewe,
Ee Bwana Uliye Juu Sana.

223 Baba wa Mbinguni, jua linapotua jioni, ndege robini wanakusanyika mitini pamoja na wapenzi wao. Ndege wote wanaenda kwenye viota vyao. Hua wanarukia kwenye nyaya, juu, nyoka wasije wakawasumbua usiku kucha. Wameketi pale na kunong'onezana mpaka wanashikwa na usingizi. Ndipo jua hatimaye linatua.

224 Siku moja tunashuka kuja kwenye saa hiyo. Kutua kwa jua kutatukia. Sijui ni lini, Bwana. Bali wapo watu hapa usiku wa leo ambao wameshawishika ya kwamba wamekosea, nao wanataka kufika mahali hapo . . . Kama vile Lincoln alivyopafikia alipokuwa akifa, akasema, "Geuzeni uso wangu kuelekea kwenye machweo ya jua." Naye akaanza, "Baba yetu uliye Mbinguni."

225 Kama Moody wa kale alivyosema, "Ati hii ni mauti? Hii ndiyo siku yangu ya kutiwa taji."

226 Ee Wewe Uliye wa Milele, wapokee hivi sasa; kwa imani, wakiwa wameketi pale vitini mwao. Ulibisha moyoni mwao, kitini. Hiyo ndiyo madhabahu yao. Huu ndio wakati kwa Wewe kuwapokea, sasa hivi. Wewe ulisema, "Yeye anijiaye Mimi, sitamtupa nje kamwe."

227 Na siku moja wakati jua litakapokuwa likitua, mke ama mume anasimama karibu na kitanda, madaktari waliondoka wakaenda zao. Ee Mtakatifu, Mtakatifu, ukimya huo mzuri, mtamu, kabla tu ya kutua kwa jua. Wakati tungeweza kuinuka na kusema:

Kutua kwa jua na Nyota ya Jioni,
Na wito wangu mmoja dhahiri;
Na jalia kusiweko na kilio hukumuni
Nitakapoelekea baraharini.

228 Ee Mungu, wajalie kwenye saa hii; wakati wakingoja, wakiingojea baraka ya Mungu iwajie. Waondolee hasira yote, ulimwengu wote, mbali kabisa nao, uwaumbie moyo mpya ndani yao. Wewe ulisema, "Nitaondoa moyo wa kale, na kuwawekea moyo wa nyama. Kisha nitaweka Roho Yangu katika moyo huo, nao watatembea katika maagizo Yangu na kuzishika Amri Zangu." Kwa sababu, ni agizo la upendo, wala si la jukumu. Ni la upendo. Na upendo unatuhimiza kufanya jambo hilo. Ni jukumu la upendo, kutuhimiza. Ni jukumu letu kufuata upendo. Nami ninaomba, Mungu, ya kwamba utautoa kwa kila moyo ulioinua mkono wao usiku wa leo.

229 Na hao ambao hawakuinua mkono wao, jalia sasa, kwa neema, wainue mikono yao na kukukubali Wewe, na kujazwa na Roho Wako katika njia hii ya upole, tamu, kimya, unyenyekevu; na wajae neema, watoke hapa wakiwa mtu aliyebadilishwa. Jinsi ndege watakavyoimba tofauti, jinsi kila mtu atakavyokuwa ni wa tofauti, baada ya saa hii, Ee Bwana Uliye Juu Sana.

> Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu Bwana Mungu wa dunia.
> Mbingu na nchi zimejaa Wewe,
> Mbingu na nchi zinakusifu Wewe,
> Ee Bwana Uliye Juu Sana.

230 Ninyi sasa huku mmeinamisha vichwa vyenu, ninyi mlioinua mikono yenu mpate kukumbukwa katika maombi, je! mnajisikia kwa namna ya kwamba Mungu amenena nanyi katika njia ambayo sasa, si kwa mhemko, bali ni kitu fulani tu ndani yenu kabisa. Unajisikia kana kwamba Mungu amekupa Uzima wa Milele? Unajisikia kana kwamba unatoka kanisani usiku wa leo mtu wa tofauti? Mngeweza kuinua mikono yenu tena usiku wa leo? Mungu akubariki, mwanangu. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki. Naam. "Nitaondoka humu kanisani, usiku wa leo, mtu mpya." Watoto wachanga waliozaliwa upya katika Ufalme wa Mungu.

231 Ni kitu gani kilichotukia? Ninajua ni utaratibu wa kuja madhabahuni. Hiyo ni madhabahu ya Kimethodisti . . . utaratibu wa Kimethodisti, ninamaanisha. Ulianzishwa katika kanisa la Methodisti, katika siku za John Wesley. Kamwe haukuwako katika siku za Biblia. "Wote walioamini waliongezwa kwa Kanisa." Unaweza kuamini po pote ulipo, huko nje mashambani, huko nje mtaani, po pote pale. Po pote, haileti tofauti yo yote, ilimradi tu utakapomkubali Kristo kama Mwokozi wako binafsi. Ni tendo la Roho Mtakatifu anayeingia moyoni mwako. Mnapomwamini Yeye, mkimkubali Yeye, mmepita toka mautini kuingia Uzimani, nanyi mnakuwa viumbe vipya katika Kristo Yesu.

> Usinipite, Mwokozi,

Sasa simameni kwa miguu yenu.

> . . . unisikie'
> Unapozuru wengine,
> Usinipite.

232 Sasa ninamtaka huyo kijana mwanamume na huyo bibi mdogo, ambaye nafikiri ni mkewe, ambaye uliinua mkono wako, ninataka uinue mkono wako tena huko nyuma; mwanangu, uliyevaa koti jekundu, na bibi huyo, ambao walimkubali Kristo kama Mwokozi wao binafsi. Kijana mwanamume huyu anayeketi hapa kwenye kiti cha magurudumu, alimkubali Kristo kama Mwokozi wake, alijisikia ya kwamba Mungu amemwokoa. Na wengine kule nyuma mlioinua mikono yenu, iinueni tena

ili kwamba watu waweze kuangalia huko, wawe na ushirika pamoja nanyi.

233 Wapeni mikono, mtu aliye karibu nao, anayesimama karibu nao. Useme, “Mungu akubariki. Karibu katika Ufalme wa Mungu, ndugu yangu, dada yangu.” Ushirika, huo ndio tunaotaka. Mungu abariki. . .Mpeni mikono kijana mwanamume huyu aliyeko hapa kwenye kiti. Bwana awe pamoja naye. Hiyo ni kweli. Tunakukaribisha katika ushirika wa Roho Mtakatifu.

234 Kama kamwe hujapata kubatizwa bado, na ungetaka kubatizwa, njoo huku na umwambie mchungaji jambo hilo. Kidimbwi hapa hata kina maji ndani yake, usiku wa leo, ukitaka kubatizwa. Kila kitu kiko tayari. (Je! mlikuwa na ubatizo, hata hivyo?. . .?. . .) Lakini kidimbwi kiko tayari, kama mtu yeyote akitaka kubatizwa. Biblia ilisema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi yenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

235 Je! mnampenda? Inueni mikono yenu. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Loo, Yeye si ni wa ajabu? Mnakifurahiaje Kitabu hiki cha Waebrania? Je! mnakipenda? [“Amina.”] Naam. Kizuri sana. Sasa, ni kurekebishwa. Loo, ni kikali kinanyoosha mambo, bali tunapenda jambo hilo. Hivyo ndivyo tunavyotaka kiwe. Hatukitaki kiwe namna nyingine.

236 Sasa, je! unaamini Paulo alipata mamlaka kuhubiri Hilo namna hiyo? Paulo alisema, “Kama Malaika akija na kuhubiri injili nyingine yoyote, na alaaniwe.” Hiyo ni kweli? Kwa hiyo tunampenda kwa moyo wetu wote.

237 Sasa nitamwomba mchungaji aje hapa kwa muda kidogo tu, ndugu yetu mpendwa sana, Ndugu Neville, naye atakuwa na neno la kuwaambia. Na sasa, Bwana akipenda, tutawaona Jumatano usiku, na kufanya matayarisho kuhusu kwenda kwa Ndugu Graham Snelling kwa ajili ya usiku wa kusanyiko. Na halafu kwa ajili ya mahubiri hapa ya kuendelea, na mlango wa 7 na wa 8, Jumatano hii ijayo usiku. Ndugu Neville.

KITABU CHA WAEBRANIA

Jumbe hizi kumi na moja za Ndugu William Marrion Branham zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza kutoka tarehe 21 Agosti mpaka tarehe 22 Septemba, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, U.S.A., zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org